# MCHANGO WA ANDANENGA KATIKA USHAIRI WA KISWAHILI

Na

Salum Abdallah Kanema

Tasnifu iliyowasilishwa Kwa Ajili ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Uzamili ya Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu Cha Dodoma

Chuo Kikuu Cha Dodoma

Oktoba, 2015

## ITHIBATI

Aliyesaini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma na anapendekeza tasnifu hii inayoitwa ***Mchango wa Andanenga Katika Ushairi wa Kiswahili*** ikubaliwe kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Sanaa ya Lugha katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

………………………………

Dkt. Muhammed Seif Khatib

Msimamizi

Tarehe……………………………

## IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi **Salum Abdallah Kanema** ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi, na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili au Shahada yoyote.

Saini……………………………

Salum Abdallah Kanema

Tarehe…………………………

Hairuhusiwi kuiga, kurudufisha, kutafsiri, kunakili, wala kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa namna yeyote ile bila idhini ya maandishi ya Mtafiti au Chuo Kikuu cha Dodoma.

## SHUKRANI

Nianze kwa kumshukuru Allah muumba ardhi na mbingu mwenye uwezo usiomithilika kwa kunileta katika dunia hii kupitia wazazi wangu. Pumzi na siha njema aliyonijaalia imeniwezesha katika kukamilsha tasnifu yangu. Lakini pia kwa kuniwezesha tunuku ya kufikia kiwango hiki cha kitaaluma.

Namshukuru mwalimu na mjomba wangu, Jabir Joseph Masenga aliyenifundisha somo la Kiswahili shule ya upili Bagamoyo kwa kunijengea msingi mzuri na imara wa kitaaluma hasa katika somo la Kiswahili. Alikuwa akituhamasisha darasani kwa kutwambia kuwa: ***"…someni sana Kiswahili kwani Kiswahili kina kesho"***. Kadhalika, nawashukuru wale wote walionitia moyo kwa namna ya pekee katika kuikamilisha tasnifu hii ambayo kila kukicha walinishauri nisikate tamaa katika kuikamilisha kazi hii. Ama hakika uungwana ni vitendo. Hapa sitakuwa muungwana kama sitawataja kwa uchache ili kuwakilisha wengine.

Kwanza, namshukuru kwa namna ya pekee msimamizi wangu Daktari Muhammed Seif Khatib. Mungu hugawa vipawa na karama tofauti kwa watu wake. Daktari amejaaliwa kipawa cha kufundisha hatua kwa hatua. Tangu mwanzo wa utafiti huu alikuwa dira yangu kuu. Hakuchoka nilipohitaji msaada na maelekezo yake bila kujali majukumu yake mengine ndani ya Chama chake na Serikali. Alinisaidia kwa dhati ya moyo wake. Hakika naona fahari na najivunia kusimamiwa naye kwani nimechota na kugida ujuzi wake wa kutosha ingawa mara zote nazi haishindani na jiwe. Namshukuru kwa kunipatia kata ya maji wakati nilipokuwa nataka kukata kiu ya ujinga na, hatimaye kupata mwanga wa maarifa. Namuombea uzima kwa Allah, amjalie maisha marefu yenye siha njema na hatimaye wanataaluma wengine

waendelee kunywa maji hayo ya pekee ili kumaliza kiu zao za taaluma. Daktari, namaliza kwa kusema nakushukuru sana.

Shukrani zangu pia zimwendee mke wangu kipenzi, Lila Amir Massawe, kwa uvumilivu na ushauri wake kwangu. Nilipochoka, alinishajiisha na alinishauri nisikate tamaa. Namshukuru kwa msaada wake wa hali na mali wakati wa uandishi wa tasnifu hii. Alikuwa karibu sana na mimi katika kuhakikisha kazi hii inakamilika. Mungu akubariki sana mke wangu. Amedhihirisha bayana kuwa mke ni nguzo ya nyumba. Uvumilivu na upendo wake kwangu vimeniwezesha kutamatisha tasnifu hii. Tasnifu hii si yangu pekee, bali pia ni tunu na zawadi kwake mke wangu kipenzi.

Shukrani hizi hazitakamilika bila kuwashukuru ndugu zangu wote kwa kunitia moyo wakati wa uandishi wa tasnifu hii. Hususan Michael Bernad, Salum Papeni, Saidi Mtanda (Mbunge) na Muhusin Shariff hawa walikuwa msaada mkubwa kwangu katika kuikamililisha kazi hii hasa pale ninapotingwa na kuchoka. Nawashukuru sana kwa mchango wao wa hali na mali katika kufanikisha kazi hii. Mungu atufungamanishe daima.

Nitakuwa mwizi wa fadhila nisipomshukuru Daktari E.F.K Chiduo, mhadhiri wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wakutubi wa Maktaba na Makavazi ya TATAKI kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika kupata marejeleo kwa ajili ya utafiti huu. Mungu amzidishie moyo yeye na wanataasisi wake.

Kipekee nawashukuru wazazi wangu wapendwa Abdallah Salum Kanema, mkewe Fatuma Kejeli Mwintanga pamoja na Mbaruku Idd Janja (marehemu) na mkewe

Fatuma Idd Mkuda.  Nawashukuru sana wazazi wangu. Mungu awape maisha marefu.

Nawashukuru pia wanafunzi wenzangu wa Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Sanaa ya Lugha katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma mwaka 2011/2012 kwa ushirikiano wao wa kimawazo tangu mwanzo wa tasnifu hii. Sitamsahau Suleiman Mvomvo na Gervas Kasiga kwa mawazo na ushauri tulioshirikiana ili kuboresha kazi hii.

Mwisho, siyo kwa kutokuwa umuhimu, namshukuru mzee Andanenga na familia yake kwa kuniwezesha kupata data na dondoo muhimu kuhusu utafiti huu. Hakika michango na mawazo yao ilikuwa muhimu katika kuifanya na kuikamilisha kazi hii.

## TABARUKU

Kwanza, kwa mwenyezi Mungu
Muumba ardhi na mbingu
Yeye kimbilio langu
Kwa siha kunijalia.

Pili, ni kwa mke wangu
Johari wa moyo wangu
Lila laazizi wangu
Mengi umevulimilia.

Tatu, kwa wazazi wangu
Hawa ndiyo nguzo kwangu
Nawaombea kwa Mungu
Vizuri wamenilea.

Mwisho kwa walimu wangu
Walikuwa dira kwangu
Hawakufanya mizungu
Elimu kunipatia.

## IKISIRI

Tasnifu hii, imejikita katika kuangalia na kuchunguza mchango wa Andanenga katika ushairi wa Kiswahili. Tasnifu hii imejielekeza zaidi katika kuangalia na kuchunguza mchango wa kidhamira na kimuundo katika ushairi wa mwandishi huyu. Kuna mchango mkubwa wa ushairi wa Andanenga katika ushairi wa Kiswahili, lakini tafiti na tahakiki za kina hazijafanyika bado juu ya mshairi huyu mwenye ulemavu wa macho. Ingawa tafiti na tahakiki nyingi zimefanywa kuhusu ushairi wa Kiswahili na maisha ya washairi, bado tafiti na tahakiki nyingi hazijamuangalia kwa jicho yakinifu mshairi huyu. Kutokana na hilo, mtafiti wa kazi hii aliona kuna haja ya kufanya utafiti kwa kina zaidi ili kubaini mchango wa mwandishi huyu katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili hasa katika kubaini mchango wake wa kidhamira na kimuundo katika ushairi wa Kiswahili. Lakini pia kuna haja ya kujua mbari yake na maisha ya mshairi huyu. Asilimia kubwa ya utafiti huu ulifanyika maktabani na udurusi wa vitabu teule vya mwandishi huyu ambavyo ni *Diwani ya Ustadh (1993)* na *Bahari ya Elimu ya Ushairi (2002).* Kadhalika mtafiti pia alikwenda uwandani kukutana na baadhi ya watu wa karibu wa mtafitiwa na kuhojiana na mtafitiwa mwenyewe. Pia, baadhi ya maeneo ikiwemo TATAKI ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilitembelewa ili kupata taarifa zaidi. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa Andanenga ana mchango mkubwa katika ushairi wa Kiswahili kidhamira na kimuundo. Kidhamira, yanaonekena mambo mengi yaliyojadiliwa na mshairi huyu katika mashairi yake yanasadifu na kuhalisika katika maisha ya kila siku ya jamii ya Watanzania. Kimuundo, ameweza kubainisha miundo changamani ya ushairi wa Kiswahili na kupata mitindo anuai katika ushairi huu. Ameonesha ustadi wake katika usanaji wa miundo na mitindo ya ushairi wa Kiswahili, ya zamani, ya sasa na mipya hivyo kuupa hadhi ushairi huu.

# YALIYOMO

ITHIBATI .......... i
IKIRARI NA HAKIMILIKI .......... ii
SHUKRANI .......... iii
TABARUKU .......... vi
IKISIRI .......... vii
VIAMBATISHO VYA TAARIFA ZA ANDANENGA .......... xi
ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA .......... xiii
ORODHA YA PICHA ZILIZOTUMIKA .......... xi
YALIYOMO .......... viii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI .......... 1**
1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti .......... 1
1.2 Historia ya Maisha ya Amiri Sudi Andanenga .......... 2
1.2.1 Ukoo na Kuzaliwa Kwake .......... 2
1.2.2 Ndoa na Watoto .......... 4
1.2.3 Kuhusu Ulemavu wa Macho .......... 5
1.2.4 Maswala yake ya Kielimu na Kazi .......... 6
1.2.6 Ushairi wa Kimapokeo .......... 9
1.2.7 Tuzo na Mashindano .......... 11
1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti .......... 13
1.4 Malengo ya Utafiti .......... 14
1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti .......... 14
1.4.2 Malengo Mahususi .......... 15
1.5 Tija na Umuhimu wa Utafiti .......... 15
1.6 Maswali ya utafiti .......... 15
1.7 Mawanda ya Utafiti .......... 16
1.8 Mpango wa Tasnifu .......... 16

**SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO .......... 17**
2.1 Utangulizi .......... 17
2.2 Dhana ya Ushairi .......... 17

2.2.1 Dhana ya Muundo katika Ushairi ..................................................................... 20
2.2.2 Dhamira katika Ushairi ......................................................................................... 21
2.3 Mapitio ya Kazi za Andanenga ............................................................................. 23
2.4 Hitimisho................................................................................................................. 25

**SURA YA TATU:MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI ....................................... 26**
3.1 Utangulizi ................................................................................................................. 26
3.2 Uchambuzi wa Data ............................................................................................... 26
3.3 Mbinu za Kukusanyia Data ................................................................................... 26
3.4 Mbinu za Kupata Sampuli....................................................................................... 27
3.4.1 Sampuli ya Watafitiwa ......................................................................................... 27
3.4.2 Mahali pa Utafiti ................................................................................................... 27
3.5 Nadharia za Utafiti ................................................................................................. 28
3.6 Hitimisho................................................................................................................. 32

**SURA YA NNE:UCHAMBUZI NA UCHANGANUZI WA DATA ZA UTAFITI ................................................................................................................. 33**
4.1 Utangulizi ................................................................................................................. 33
4.2 Maelezo kuhusu Vitabu Teule ............................................................................... 33
*4.2.1 Diwani ya Ustadh.................................................................................................. 33*
4.2.2 Bahari ya Elimu ya Ushairi .................................................................................. 35
4.3 Mchango wa Kidhamira wa Andanenga katika Ushairi wa Kiswahili .............. 36
4.3.1 Mchango wa Kimuundo wa Andanenga katika Ushairi wa Kiswahili ........... 53
4.4 Hitimisho................................................................................................................. 82

**SURA TA TANO : MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ......... 83**
5.1 Utangulizi ................................................................................................................. 83
5.2 Muhutasari wa Utafiti ............................................................................................. 83
5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ......................................................................... 84
5.4 Mchango wa Utafiti................................................................................................. 86
5.5 Maoni ya Mtafiti ..................................................................................................... 87
5.6 Mapendekezo kuhusu Tafiti Zijazo....................................................................... 87
5.7 Hitimisho................................................................................................................. 88

MAREJELEO ........................................................................................................ 89
VIAMBATISHO.................................................................................................... 93

## ORODHA YA PICHA ZILIZOTUMIKA


Kilelezo Na 1: Mshairi Amir Sudi Andanenga. Chanzo: Data za utafiti (2014). ..... xiv

Kilelezo Na 2: Andanenga akiwa nyumbani kwake Kinondoni Shamba, Dar es Salaam.Chanzo: Data za utafiti (2014). ............................................ 3

Kilelezo Na 3: Mke wa Andanenga, Tatu binti Saadala. Chanzo: Data za utafiti (2014). ............................................................................................ 4

Kilelezo Na 4: Andanenga akiwa na binti yake Nadhija na mjukuu wake Faridi ambaye ni Mtoto wa Nadhija.Chanzo: Data za utafiti (2014). .......... 5

Kilelezo Na 5: Nyumba ya Andanenga, Kinondoni Shamba, Dar es Salaam. Chanzo: Data utafiti (2014). ............................................................................ 7

Kilelezo Na 6: Mtafiti akiwa na Andanenga na baadhi ya tuzo za mshairi huyo. Chanzo: Data za utafiti (2014). ..................................................... 11

Kilelezo Na 7: Tuzo ya zeze mwaka 2002. Chanzo: Data za utafiti (2014). ............. 12

Kilelezo Na 8: Tuzo ya nguli wa ushairi 2003. Chanzo: Data za utafiti (2014). ....... 13

Kilelezo Na 9: Jalada la Diwani ya Ustadh (1993) Chanzo: Data za utafiti (2014). . 34

Kilelezo Na 10. Jalada la Diwani ya Bahari ya Elimu ya ushairi (2002): Chanzo: Data za utafiti. (2014) ...................................................................... 35

## VIAMBATISHO VYA TAARIFA ZA ANDANENGA

VIAMBATISHO ........................................................................................................ 93
I. Hojaji kwa ndugu, jamaa, na marafiki wa Amiri Sudi Andanenga ....................... 93
II. Hojaji kwa washairi ................................................................................................ 94
III. Hojaji kwa mtunzi mwenyewe ............................................................................. 95
IV. Baadhi ya vyeti alivyotunukiwa ........................................................................... 96
V.Orodha ya watu waliohojiwa katika utafiti huu ..................................................... 98

## ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

| | | |
|---|---|---|
| AU | : | African Union |
| BAKITA | : | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| Bw | : | Bwana |
| Dkt | : | Daktari |
| DUP | : | Dar es Salaam University Press |
| EAC | : | East African Community |
| EALB | : | East African Literature Bureau |
| EU | : | European Union |
| Ltd | : | Limited |
| M.A | : | Master of Arts |
| Mk | : | Mke |
| SADC | : | Southern African Development Community |
| TANU | : | Tanaganyika African National Union |
| TATAKI | : | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| TBC | : | Tanzania Broadcasting Cooperation |
| TPH | : | Tanzania Publishing House |
| TUKI | : | Taassisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| UAE | : | United Arabic Emirates |
| UDSM | : | University of Dar es Salaam |
| UDOM | : | University of Dodoma |
| Uk | : | Ukurasa |
| UKUTA | : | Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania |



**Kilelezo Na 1: Mshairi Amir Sudi Andanenga. Chanzo: Data za utafiti (2014).**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Wapo washairi wengi wa Kiswahili waliotunga mashairi mengi katika nyakati tofauti lakini kazi zao hazijajulikana na maisha yao yanakosa kumbukumbu. Tasnifu hii ni jitihada ya kurekebisha hali hiyo. Kwa hivyo basi, tasnifu hii imeshughulikia maisha na mchango wa Amiri Sudi Andanenga katika ushairi wa Kiswahili, kwa kuangalia mchango wake wa kidhamira na kimuundo katika vitabu vyake viwili vya *Diwani ya Ustadh* (1993) na *Bahari ya Elimu ya ushairi* (2002).

Ushairi, ni moja ya utanzu wa fasihi ya Kiswahili. Utanzu huu chimbuko lake ni fasihi simulizi na baadae fasihi andishi. Kimsingi utanzu huu wa fasihi ulianza kama ushairi simulizi, lakini kutokana na maendeleo ya hati za Kiarabu na baadaye Kirumi utanzu huu ukaanza kuandikwa katika maandishi. Chimbuko la asili la ushairi wa Kiswahili limetokana na nyimbo za jando, harusi, kazi, matambiko na kadhalika Chiraghdin (1970:7-10).

Khatib (2011:26) anadokeza kuwa, ushairi ndiyo utanzu mkongwe ukilinganishwa na tanzu nyingine za Fasihi ya Kiswahili, kama vile Tamthiliya na Riwaya. Kwa hivyo basi, ushairi ndiyo utanzu mama katika historia ya fasihi duniani. Hii ni kwa sababu wanafasihi wengi wa mwanzo walijibainisha zaidi katika utanzu huu wa ushairi, kwani hata kazi zao za mwanzo za kifasihi zilikuwa katika umbo la ushairi. Ni utanzu ambao umepitia hatua mbalimbali katika maendeleo na kukua kwake mpaka ulipo hivi sasa.

## 1.2 Historia ya Maisha ya Amiri Sudi Andanenga

### 1.2.1 Ukoo na Kuzaliwa Kwake

Amiri Abdallah Sudi Andanenga, maarufu kwa jina la ushairi *Sauti ya Kiza* alizaliwa tarehe 02/10/1936 huko Kilwa, Mkoani Lindi katika kijiji cha Kikole na kukulia katika kitongoji cha Nanyati. Andanenga anatokana na kabila la Wangindo kwa baba na mama. Baba yake ni Abdalla Sudi na Mama yake ni Khadija Abdalla Kaondo. Mwenyewe Andanenga anapenda kutumia majina yake yote, yaani Amiri bin Abdallah bin Sudi bin Abdallah Malukila Mkwenya Ndegere Niyuka Ngolwe. Kabla hajajulikana kwa lakabu ya *Sauti ya Kiza,* mshairi huyu alijulikana zaidi kwa lakabu ya ushairi ya *Andanenga.* Andanenga ni neno la Kingindo, litokanalo na mwambatano wa maneno mawili ya lugha hiyo, yaani ***anda*** ikiwa na maana ya kama na ***nenga*** ikiwa na maana ya mimi. Hivyo, kwa Kiswahili neno hilo maana yake ni "Kama Mimi". Lakini baada ya kupata matatizo ya macho yaliyomsababishia upofu mpaka hii leo, mshairi huyu akapachikwa lakabu ya *Sauti ya kiza* na huku jina la Andanenga limekuwa sehemu ya jina lake halisi. Mama yake Andanenga, Bi Khadija binti Abdallah Kaondo Kapati wa Kikuru anatokana na kabila la Wangindo ambao asili yao ni Liwale katika mkoa wa Lindi.




**Kilelezo Na 2: Andanenga akiwa nyumbani kwake Kinondoni Shamba, Dar es Salaam.Chanzo: Data za utafiti (2014).**

Babu yake Amiri wa kukeni ni mzee Kaondo, ambaye alihamia Kilwa kutoka Liwale kwa kukimbia mkewe asije kuuawa baada ya kujifungua watoto watatu kwa pamoja. Kutokana na mila za Wangindo kwa wakati huo, hali hiyo ya kujifungua watoto watatu huchukuliwa kama mkosi na uchuro katika jamii. Hivyo, yeye na mkewe wakaamua kukimbia na wakafika Kilwa na kuselelea hapo kwa maisha yao yote.

### 1.2.2 Ndoa na Watoto

Mwaka 1963, Amiri Sudi Andanenga alifunga ndoa na mkewe kipenzi, Tatu binti Saidi Saadala ambaye anaishi naye mpaka hivi sasa nyumbani kwao Kinondoni Shamba jijini Dar es Salaam.



**Kilelezo Na 3: Mke wa Andanenga, Tatu binti Saadala. Chanzo: Data za utafiti (2014).**

Katika ndoa yao wenza hawa wamebahatika kupata watoto tisa ambao ni Sudi, Saidi, Muhamedi, Malukila, Abdalla, Ngalela, Hija, Faraja na Nadhija. Kati ya hao, Sudi na

Abdalla, wameshatangulia mbele ya haki. Andanenga amebahatika pia kupata wajukuu tisa kama ilivyo idadi ya watoto wake.




**Kilelezo Na 4: Andanenga akiwa na binti yake Nadhija na mjukuu wake Faridi ambaye ni Mtoto wa Nadhija.Chanzo: Data za utafiti (2014).**

### 1.2.3 Kuhusu Ulemavu wa Macho

Mwaka 1975 Disemba, Andanenga alipata ulemavu wa macho. Tatizo hilo lilianza akiwa likizo Tunduma Mkoani Mbeya alipoenda kwa ajili ya matembezi. Aliporudi Dar es salaam macho yalimuuma kwa nguvu sana na yalipopona baadaye yakafa kabisa. Mwenyewe Amiri akiongea kwa uchangamfu alivyokuwa akifanya mahojiano na mtafiti, anadai kuwa: *"ulemavu huu wa macho umenipa uwezo*

*mkubwa wa kutunga mashairi, kufikiri zaidi na kuhifadhi zaidi na sasa nina uwezo mkubwa wa kudadavua mambo kuliko mwanzo nilivyokuwa ninaona".*

Penye miti hapana wajenzi. Andanenga hakupata mtu wa kurithi kipawa chake cha utunzi wa mashairi, si watoto si wajukuu zake. Mwenyewe anaeleza kwa masikitiko kuwa: *"kama Sudi angekuwepo hai, basi angerithi kipawa changu kutokana na mapenzi makubwa aliyokuwa nayo katika ushairi"*. Andanenga ameusia endapo atatangulia mbele ya haki, basi kazi zake za ushairi na Kiswahili pamoja na tuzo zake zitunzwe na yeyote anayependa ushairi wa Kiswahili na Kiswahili ili zije kuwa tunu kwa vizazi na vizazi.

### 1.2.4 Maswala yake ya Kielimu na Kazi

Mwaka 1949, Andanenga alipelekwa shule ya msingi Kikole huko Kilwa na kuhitimu mwaka 1956. Baada ya kufaulu mtihani wa darasa la nane Shule ya Kati ya Mtanga mwaka 1957 alichaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari ya wavulana Songea. Hakuendelea na masomo kwani wazazi wake wakati huo walishindwa kulipa karo iliyotakiwa. Hivyo basi mshairi huyu aliishia darasa la kumi. Kwa vile dhamira ya kujiendeleza kitaaluma kwa Andanenga ilikuwa ndani ya damu yake hakuchoka kutafuta elimu na kujiendeleza zaidi. Alijiunga na Chuo cha Watumishi wa Serikali hapo Magogoni Dar es Salaam na kufaulu mitihani vizuri.

Kabla ya kupofuka, mwandishi Amiri Sudi Andanenga alikuwa mtumishi katika idara na wizara mbalimbali Serikalini. Mwaka 1958 alipata kazi ya ukarani katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa. Mwaka 1959 alifanya kazi Ofisi ya Bunge akiwa Karani msaidizi. Mwaka 1961 alihamishiwa Wizara ya Mawasiliano akiwa Karani Mkuu na mwaka 1965 Andanenga alihamishiwa Wizara ya Maji. Katika Wizara hii

alifanya kazi akiwa Ofisa Mkuu wa Wizara na baadaye mwaka 1966 alikuwa muhasibu katika Wizara hiyo. Mwaka 1977 Andanenga alistaafu rasmi utumishi wa umma kutokana na maradhi ya macho aliyoyapata ghafla na hatimaye kuwa kipofu.



**Kilelezo Na 5: Nyumba ya Andanenga, Kinondoni Shamba, Dar es Salaam. Chanzo: Data utafiti (2014).**

### 1.2.5 Andanenga Mshairi

Andanenga ni mshairi wa miaka mingi tokea mwaka 1948 hadi sasa. Alianza kutambulika katika mawanda ya mashairi tokea mwaka 1954. Shairi lake la kwanza kutoka gazetini liliitwa "***Kiswahili neno "wewe"***" ambalo alilitunga akiwa darasa la sita Shule ya Kati Mtanga na kutolewa katika gazeti la Mamboleo. Hebu tunukuu ubeti wa pili wa shairi hilo, linasema:

**“Wewe” kwa mwanaadamu, si matusi naapia,**
**Ninyi neno maalumu, kila mtu alijua,**
**Kwa Kiswahili muhimu, penye wengi hutumiwa,**
**Kiswahili neno “wewe”, liwe matusi kwa nini?**

Upenzi, msukumo na mshawasha wa utunzi wa mashairi aliupata kutoka kwa mjomba wake Salum Abdalla Kaondo ambaye alikuwa akipenda kusoma mashairi katika gazeti la Mamboleo. Kadhalika, mshairi alipata hima ya ushairi kutoka kwa Saidi Ndembo Mkwawa (Vuta kamba) na Mrisho Saidi (Shindikiza). Mwaka 1959, Andanenga alihamia Dar es Salaam kutoka Kilwa alipokuja kufanya kazi katika ofisi za Bunge. Hapa alikutana na mshairi Saidi Roberts aliyejulikana kwa lakabu ya ushairi ya *Kimbunga* ambaye alimuongezea sana Andanenga hamasa katika utunzi wa mashairi.

Baada ya hapa, Andanenga akaanza kuambatana na Kaluta Amri Abeid (1924-1964), gwiji wa ushairi na mtaalamu wa Kiswahili ambaye walipendana sana. Kwa maelezo yake mwenyewe, Andanenga alidai kuwa Kaluta ndiye aliyemwathiri kwa utunzi wake kwa kiasi kikubwa sana.

Mashairi yake Andanenga yaliwavuta wengi wakiwemo maprofesa na walimu wa lugha katika vyuo. Hivyo, akawa ni mtu anayezungumzwa katika vikao na mahafali mbalimbali. Mwaka 1964 wakati wa kuadhimisha miaka kumi ya TANU, Andanenga aliingia katika shindano la kuelezea kwa nini kuna sherehe za Sikukuu ya Sabasaba ambayo ni siku iliyozaliwa TANU tarehe 7.7.1954. Katika shindano hilo, mabingwa na washairi mahiri wengi walishiriki, lakini hilo halikumfanya Andanenga ashindwe kushindana. Hivyo, aliibuka mshindi wa kwanza katika shindano hilo na kupewa zawadi ya shilingi mia. Wa pili, alikuwa ni Muhamed Selemani (Mtu Chake)

wa Dar es Salaam na watatu alikuwa ni Akilimali Snowhite wa Kigoma. (Mahojiano na mtafiti, 13/6/2013).

Andanenga ametunga mashairi mengi sana kiasi ambacho hata yeye mwenyewe hakumbuki idadi yake kamili. Mpaka sasa mshairi huyu ameshatoa vitabu viwili ambavyo ni *Diwani ya Ustadh (1993)* na *Bahari ya Elimu ya Ushairi (2002).* Lakini pia anayo miswada ya ushairi wa Kiswahili ambayo mingine imeandikwa katika maandishi ya Kibreili (maandishi nundu ya watu wenye ulemavu wa macho).

### 1.2.6 Ushairi wa Kimapokeo

Andanenga ni mfuasi na muumini thabiti wa mashairi ya kimapokeo ambayo yanafuata arudhi zote za ushairi wa Kiswahili na kupinga mtindo wa mashairi ya kisasa. Andanenga kwa mawazo yake, anaamini kuwa ushairi huu wenye kufuata vina na mizani ulianza kwa Muyaka bin Haji ambaye alianzisha utunzi wa mashairi ya vina, mizani na muwala. Ingawa ushairi wa kimapokeo ulianza zamani na Muyaka aliyakuta na kuyafata (maoni ya mtafiti).

Amiri Sudi Andanenga anauelezea ushairi wa Kiswahili kuwa ni sawa na somo linaloendana na Kiswahili chenyewe. Hivyo, anashauri kuwa watu watuunge mashairi kwa kuzingatia utanashati wenyewe wa lugha ya Kiswahili. Hapa Andanenga ananukuu shairi la Kaluta linalosisitiza kauli yake, ambalo linalosema:

**Kiswahili tusanifu, sarufi nazo tupange,**
**Ushairi kifikifu, wa kila nui tutunge,**
**Utukuke utukufu, wa nathari tuuchunge,**
**Kiswahili tukijenge, mjengo ukipasao.**

Wakati fulani, mtafti alipofanya mahojiano nyumbani kwake tarehe 15/05/2014 akiwa mgonjwa kitandani, Andanenga alisema: *"ushairi wa Kiswahili kamwe*

*hautakufa, utaendelea kuwepo na Kiswahili chake, maadamu watunzi mahiri wa zama hizi wapo na ushairi unaandikwa, basi ushairi wa Kiswahili utadumu daima. Siku nitakapoondoka ulimwenguni basi watu wanikumbuke na mimi kwa ushairi wangu".* Hapo hapo kitandani akiwa na uchovu sana, akatongoa hivi:

**Kuna siku pindi mwaka, safari nitasafiri**
**Safari isiyo shaka, safari hiyo safari**
**Wengi imeshawafika, inikoseje Amiri?**
**Sanaa ya ushairi, uwe ndo wakili wangu.**

Kwa maoni ya Andanenga anamwona Daktari Muhammed Seif Khatib kuwa ndiye mshairi pekee aliyebaki katika kuuhami na kuutetea ushairi andishi wa Kiswahili kwa zama hizi. Kwa vile anaonekana kuwa na dhamira ya dhati katika kuuhami ushairi andishi wa Kiswahili, lakini pia hata kuwaenzi na washairi wenyewe. Andanenga ni mwana UKUTA. Aliingia UKUTA mwaka 1960 akiwa na magwiji wa ushairi wa wakati huo kama vile Saadani Kandoro, Shaaban Robert na wengineo wengi yeye akitumikia katika ngazi kadha wa kadha ndani ya chama hicho. Andanenga anasema kuwa kwa sasa ingawa UKUTA umeporomoka lakini upo katika harakati za kujengwa upya.



**Kilelezo Na 6: Mtafiti akiwa na Andanenga na baadhi ya tuzo za mshairi huyo.**

**Chanzo: Data za utafiti (2014).**

### 1.2.7 Tuzo na Mashindano

Andanenga ameshiriki mashindano mengi ya ushairi na ameshinda mengi yakiwemo ya Kitaifa na Kimataifa na kupata tuzo mbalimbali. Baadhi ya tuzo hizo ni pale mwaka 1964 alipotunukiwa cheti na ‘Tanganyika National Festival’ akiwa mshindi wa kwanza. Aidha aliinyakua tuzo ya Zeze mwaka 2002 inayotolewa na Mfuko wa Utamaduni Tanzania. Mwaka 2003 alipewa ‘Certificate Of Merits’ akiwa nguli wa ushairi kwa mchango wake mkubwa wa lugha ya Kiswahili. Mwaka 2005, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam idara ya TUKI sasa TATAKI, ilimtunuku cheti cha heshima mshairi huyu kwa kuthamini na kutambua mchango wake mkubwa katika kukieneza, kukikuza, kukiimarisha na kukienzi Kiswahili.



**Kilelezo Na 7: Tuzo ya zeze mwaka 2002. Chanzo: Data za utafiti (2014).**

Andanenga ni mshairi hodari na makini katika utungo wa malumbano. Pia yeye ni mwimbaji na hivyo BAKITA iliwahi kumwomba kuimba utenzi maarufu wa *Inkishafi* uliotungwa huko Pate na A. Nassir. Aliuimba kwa ghibu na kurikodiwa katika kanda kama hazina bora ya utamaduni wa Kiswahili.



**Kilelezo Na 8: Tuzo ya nguli wa ushairi 2003. Chanzo: Data za utafiti (2014).**

### 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Ushairi wa Kiswahili umeandikwa na washairi tofauti katika maeneo na nyakati mbalimbali. Ushairi huo umekuwa na maudhui na mawanda anuai. Hata hivyo, maisha, wasifu na mashairi ya washairi wengi yamekosa nafasi ya kuandikwa na kuchambuliwa. Habari za maisha ya washairi, tabaani hutoa mchango muhimu katika kuelewa undani wa maudhui na mbinu nyingine za kisanaa katika ushairi wa Kiswahili.

Ushairi wa Kiswahili katika uhai wake kwa kiasi fulani umeshughulikiwa na wahakiki na watafiti mbalimbali wa Tanzania na nje ya Tanzania ambao hutusaidia kupata taaluma. Wataalamu hao kadhaa pia wamefanya tafiti juu ya maisha ya washairi na kazi zao za kishairi. Miongoni mwa tafiti hizo ni pamoja na ya Muyaka (Abdulazizi, 1973), Malenga wa Karne Moja (Chiraghdin na Nabahany, 1987), Inkishaf (Gibbe, 1995), Jawabu la Mwanakupona (El-Maawy, 2011) na Kale ya Washairi wa Pemba (Abdilatif, 2011) na wengine kadha wa kadha.

Hata hivyo, pamoja na kuwepo bidii, ari na jitihada za kuutafiti ushairi wa Kiswahili na washairi wake, bado kuna baadhi ya washairi mahiri katika uga huu na hawakuweza kufanyiwa utafiti kabisa na wapo wale ambao walau wametajwa juu juu hapa na pale. Kwa upande wa mshairi Andanenga, bado tahakiki, uchunguzi na utafiti wa kina wa mshairi huyu haujafanywa kabisa. Wahakiki na watafiti mbalimbali wa ushairi wa Kiswahili baadhi yao wamekuwa wakimwangalia juu juu na kumtaja hapa na pale mshairi huyu.

Upungufu huo ndiyo uliomfanya mtafiti wa kazi hii kushughulikia kwa mapana na marefu mchango wa Amir Sudi Andanenga katika mwelekeo wa kuendeleza ushairi wa Kiswahili.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

### 1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Kushughulikia mchango wa Andanenga katika ushairi wa Kiswahili.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

Malengo mahususi ya utafiti huu yamejikita katika kubaini mambo yafuatayo:

i. Kubainisha mchango wake wa kidhamira katika ushairi wa Kiswahili.

ii. Kubainisha mchango wake wa kimuundo katika ushairi wa Kiswahili.

## 1.5 Tija na Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ni muhimu kwa vile umebainisha mchango wa Andanenga katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili. Mchango huu unatarajiwa kuwa sehemu ya kukuza lugha, sanaa na aina ya mitindo na miundo ya ushairi wa Kiswahili.

Utafiti huu unatarajiwa kuchochea ari, hamu na haja ya tafiti nyingine zaidi katika nyanja nyingine za ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu utakuwa chachu ya kuibua washairi wengine ambao nao wana mchango mkubwa katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili. Nataraji kazi hii imeongeza maktaba na makavazi ya ushairi wa Kiswahili.

## 1.6 Maswali ya utafiti

Maswali ya utafiti yalikuwa mawili ambayo yanatokana na malengo mahususi ya utafiti.

i. Nini mchango wa Amiri Sudi Andanenga katika ushairi wa Kiswahili kidhamira?

ii. Kwa kiasi gani Amiri Sudi Andanenga amekuwa na mchango mkubwa wa kimuundo na mtindo katika ushairi wa Kiswahili?

## 1.7 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu umeshughulikia mchango wa Andanenga katika ushairi wa Kiswahili kidhamira na kimuundo. Utafiti umejikita zaidi katika kuzizamia diwani zake mbili ambazo ni *Diwani ya Ustadh (1993)* na *Bahari ya Elimu ya Ushairi (2002*). Tumevishughulikia vitabu hivi kwa kuwa ndivyo vilivyochapwa na kufahamika katika uga wa ushairi andishi wa Kiswahili. Hata hivyo, kazi zake nyingine za ushairi hata zilizo katika miswada, majarida au magazeti zimetumika kutoa ithibati katika kuchambua mchango wake katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili.

## 1.8 Mpango wa Tasnifu

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya kwanza inahusu utangulizi juu ya mada husika katika utafiti. Katika sura hii mambo yaliyojadiliwa ni pamoja na usuli, historia ya maisha ya Andanenga, tamko la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, mawanda ya utafiti na umuhimu wa utafiti.

Sura ya pili inahusu mapitio ya machapisho na maandiko mbalimbali kuhusu kazi husika na baadhi ya mapitio ya kazi za Andanenga.

Sura ya tatu ya tasnifu hii inahusu mbinu za utafiti zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data za tasnifu hii. Lakini pia kuangalia mbinu za kupata sampuli, sampuli ya watafitiwa, mahali pa utafiti na nadharia za utafiti.

Sura ya nne imechambua, imejadili na kubainisha data kuhusu mchango wa kidhamira na kimuundo wa Andanenga katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili. Imebainisha pia matokeo ya utafiti na ufafanuzi umetolewa ili kujenga mjadala kuhusu mchango wa kidhamira na kimuundo wa Andanenga katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili. Sura ya tano ni hitimisho na mapendekezo kwa ajili ya tafiti za baadae.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.1 Utangulizi

Sehemu hii imepitia maandiko mbalimbali yanayojadili dhana ya ushairi na ushairi wa Kiswahili kwa sababu mada hiyo inahusu maandiko ya Andanenga na mashairi yake. Lengo kuu ni kuangalia miundo na maudhui yanayojitokeza.

## 2.2 Dhana ya Ushairi

Kuhusu dhana ya ushairi kwa jumla wataalamu kadha wa kadha wametoa maoni yao katia mielekeo tofauti.

Warren na Wellek (1985:36) wanasema kuwa:

> *"…ushairi ni utungo utumiao mfumo maalumu wa maneno katika kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Ujumbe unaweza kuwa wa furaha, huzuni au masimulizi".*

Kwa mtazamo wa mshairi na mtaalamu mwingine yeye kwake: Ushairi umekuwa chombo muhimu katika kuhifadhi historia, falsafa na utamduni wa jamii (Sanka, 1994:2). Anaongeza kwa kusisitiza mtaalamu huyu kuwa; ushairi ni zao la jamii husika na hivyo kuwa na sifa maalumu kulingana na muktadha lengwa kwa jamii husika.

Kwa upande wake Olson (1975:32-37) anauelezea ushairi wa Kiswahili kama chombo cha kuhamasisha matarajio na matamanio ya Waswahili na jamii kwa jumla katika kujiletea maendeleo. Pia anaendelea kuelezea kuwa ushairi wa Kiswahili umechukua nafasi kubwa kama chombo cha mawasiliano baina ya wanajamii. Kwa mfano kwake yeye kama mshairi endapo analiona jambo ndani ya jamii yake na

haridhiki nalo kwa namna lilivyo au lifanywavyo, basi hutunga shairi kuelezea jambo hilo. Washairi wengi wenye mawazo ya kimaendeleo hufanya hivyo.

Mulokozi na Kahigi (1974:25) wawili hawa nao wanasema kuwa:

> *"…ushairi ni sanaa iliyopambanuliwa kwa sanaa maalumu ya maneno fasaha yenye muwala, kwa lugha ya mkato, picha, sitiari au ishara katika usemi, maandishi au mahadhi ya wimbo ili kuelezea wazo au mawazo, kufunza na kuelekeza tukio au hisi fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu kwa njia inayogusa moyo".*

Msisitizo wa wataalamu hawa kimaudhui ni kuwa ushairi andishi waweza kufunza na kutoa maonyo kutokana na wakati na mazingira ya jamii husika. Kutokana na mada hii ya utafiti imejikita kuangalia dhamira za mwandishi huyu, basi ni dhahiri dhamira hizo zitatuongoza katika kupata maonyo na mafunzo mbalimbali.

Mwandishi maarufu na gwiji wa fasihi na ushairi wa Kiswahili Shaaban Robert (1958:37) akitilia uzito katika fani ya ushairi, anasema:

> *"…ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi na tenzi. Zaidi ya kuwa sanaa ya vina, ushairi una ufasaha wa maneno macheche au muhutasari. Mawazo, maono na fikra za ndani zinapoelekezwa kwa muhutasari wa ushairi huvuta moyo kwa namna ya ajabu".*

Katika uga wa fasihi ya Kiswahili, maana ya ushairi imefafanuliwa na wataalamu mbalimbali kila mmoja akijiegemeza katika mtazamo wake. Wapo waliojiegemeza katika mtazamo wa ushairi wa kisasa na wengine katika mtazamo wa ushairi wa kimapokeo. Hali hiyo imefanya kusiwe na tafsiri na maana moja ya ushairi.

Kambi moja yenye wanafasihi vijana na wasomi wakiwemo Mulokozi na Kahigi (1974:25), kezilahabi (1973:60) na Topan (1971) walijiegemeza katika kambi ya ushairi wa kisasa. Kambi hii inasisitiza kuwa ushairi unao muundo tofauti na nathari.

Ushairi hutoa picha, sitiari, taswira, lugha ya mkato na huwa na mapigo na mpangilio maalumu. Kambi hii inaona urari wa vina na mizani siyo vitu muhimu au uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili. Kwani hizo ni sifa za ziada.

Kambi nyingine ya ushairi wa Kiswahili ni ile inayosisitiza kuwa ushairi wa Kiswahili lazima uwe na mizani na urari wa vina. Kambi hii inaongelea juu ya umuhimu wa hisi, mnato wa lugha na uzingativu wa arudhi katika ushairi wa Kiswahili. Kambi hii imeundwa na washairi kama; Mnyampala (1965: i), Mayoka (1986:3-5), Robert (1958:37), Abedi (1954:1) na Shariff (1975:70).

Mgawanyiko hapa upo waziwazi kuwa wataalamu wa kambi ya kwanza ya wataalamu Mulokozi, Kahigi, Topan na Kezilahabi na wenzao wanao mrengo wa ushairi wa kisasa. Wao hawatilii mkazo urari wa vina na mizani katika ushairi wao kuwa ndiyo msingi wa ushairi wa Kiswahili. Tofauti na wale wa kimapokeo akina Mnyampala, Robert, Abedi, Mayoka na Shariff ambao kwao urari wa vina na mizani ndiyo uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili.

Tofauti ya mitazamo yao, ndiyo iliyosababisha kuibuka kwa mgogoro mkubwa katika ushairi wa Kiswahili. Mgogoro huu ulizua kambi mbili za wanamapokeo na wanausasa. Hata hivyo, mgogoro huo ulitoa changamoto katika uwanja wa ushairi na kuwa sehemu ya mijadala ya kitaaluma na maendeleo ya ushairi wa Kiswahili.

Andanenga akiwa mlengwa wa utafiti huu yeye anajiegemeza katika kambi ya ushairi wa kimapokeo (2001:47). Utafiti huu mbali na kuangalia historia ya maisha ya Andenenga umeangalia pia mchango wake katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili ambao kwake unafata mrengo wa kimapokeo.

Hata hivyo, kwa maoni ya mtafiti anauona ushairi kuwa ni sanaa ya lugha ya mkato na mnato yenye ubunaji wa hali ya juu inayosawiri kuonesha au kueleza jambo, hisi au hali kwa namna yenye kuvuta hisia katika mpangilio mahususi wa maneno yenye urari wa vina na mizani. Kwa vile muktadha wa kazi hii umeangalia dhamira na miundo anuai katika ushairi wa Andanenga, mtafiti anaona kuwa dhana zote za wataalamu hao zipo kwa lengo la kuuendeleza na kuuenzi ushairi wa Kiswahili kwa vizazi vijavyo.

### 2.2.1 Dhana ya Muundo katika Ushairi

Baada ya kupitia maandiko machache yanayoonesha dhana ya ushairi, sasa tuangaliye maandiko yanayohusu muundo katika ushairi. Alipokuwa akifafanua dhana ya muundo wa kazi za kifasihi kwa jumla, Senkoro (2011:23-24) alisema kuwa kuna aina nyingi ya muundo hutokana na umbo la kazi ya fasihi kwa jumla. Hata hivyo, kwa upande wa ushairi wa Kiswahili, yapo mashairi yenye miundo mbalimbali iainishwayo pamoja na idadi ya mistari (vipande/mishororo) katika kila ubeti, mathalani mashairi ya uwili, utatu, unne na kadhalika. Uainisho hapa upo katika ushairi wa kimapokeo.

Senkoro ametuongoza kuweza kubaini miundo anuai yenye mshabaha katika ushairi wa Andanenga na kuweza kukidhi lengo mahusus la tasnifu hii.

Naye Mulokozi (1989:50-51) anaeleza kuwa: miundo katika ushairi wa Kiswahili ipo mingi. Baadhi ya vipengele vya muundo vinavyotumika zaidi ni mistari, beti, mizani na vina. Urefu wa mistari wakati mwingine hutofautiana kutegemea mizani ya shairi linalohusika au kutegemea mtiririko wa wazo au hisia kama ni shairi la huria. Urefu wa beti hutegemea idadi ya mistari katika kila ubeti. Zipo tungo za utatu *(tathlitha),*

unne *(tarbiya)*, na utano *(takhmisa)* na kadhalika. Mpangilio wa vina na mizani upo wa aina nyingi.

Mashairi kwa kawaida yana miundo mbalimbali kutegemea na ufundi wa mshairi mwenyewe. Katika muundo, aghalabu tunaangalia kile kinachoonekena kwa nje. Kwa mfano: mgao wa vipande, idadi ya mistari katika kila beti, kiitikio au mkarara au kibwagizo na idadi ya beti katika shairi (Masebo, 2002:38).

Kwa hiyo, msisitizo tunaopata hapo ni kuwa katika mashairi tuna miundo mbalimbali ambayo hutumiwa kuainisha mashairi kwa mujibu wa idadi ya mistari katika kila ubeti. Miundo hii ndiyo hutupa mashairi ya *mathna (mistari 2), tathlitha (mistari 3), tarbiya (mistari 4), takhmisa (mistari 5), sudusia (mistari 6)* na kadhaliaka, ambayo imejitokeza katika ushairi wa Andanenga.

Maelezo ya wataalamu hawa wachache tuliyoyapitia kuhusu dhana ya muundo katika ushairi wa Kiswahili na mifano yake, imetupa mwanga na mwelekeo wa kukichambua kipengele hiki cha fani tulipokuwa tunaangalia mchango wa kimuundo wa mshairi huyu katika ushairi wa Kiswahili.

### 2.2.2 Dhamira katika Ushairi

Eneo jengine linalojadiliwa na wataalamu ni dhamira katika ushairi wa Kiswahili, ambayo baadhi ya maandiko yake yanabainishwa:

Dhamira zinaweza kujitokeza katika nyanja mbalimbali. Mtunzi mmoja anaweza kutoa taarifa tu. Mtunzi mwingine ana dhamira ya kukosoa jambo fulani alionalo kuwa baya. Wengine hutoa masahihisho ya mgongano fulani au kuelimisha ama kuelekeza.

Dhamira katika ushairi ni wazo au mawazo mbalimbali yanayojitokeza na kujadiliwa katika ushairi. Dhamira hutokana na shughuli za jamii. Kwa kawaida dhamira huweza kuwa za kisiasa, kiutamaduni au kiuchumi (Masebo, 2008:40).

Bukagile (2008:39) naye anafafanua kuwa, dhamira katika ushairi ni suala linalozungumziwa na msanii katika kazi ya ushairi. Katika kazi ya ushairi huwa kuna dhamira kuu ambayo huwa ni kiini cha kazi ya msanii lakini huwepo dhamira ndogondogo ambazo zinaenda sambamba na dhamira kuu. Wasanii wa ushairi wakati mwengine huzungumzia dhamira tofauti tofauti kama vile mapenzi na ndoa, migongano ya kitabaka, mwanamke na nafasi yake katika jamii, maadili pamoja na haki na usawa.

Akifafanua dhana ya dhamira katika ushairi, Shaaban (2009:76) anaeleza kuwa; dhamira ni kusudio au wazo kuu la mtunzi wa kazi ya ushairi. Dhamira zaidi ya moja zinaweza kujitokeza katika ushairi. Nazo huweza kujitokeza kwa namna mbalimbali. Mtunzi anaweza kuhimiza, kutoa taarifa, kukosoa na mengineyo.

Kwa hivyo, dhamira katika ushairi ni wazo kuu ambalo ndiyo hubeba msingi wote wa dhima za ushairi kama vile: kuelimisha, kukosoa, kuadabisha, kuadilisha na kuonya jamii. Dhamira hizo huakisi maisha na mazingira halisi ya jamii husika. Hivyo, mara nyingi dhamira katika ushairi hazitokani na ombwe bali hutokana na mazingira halisi ambayo mwandishi wa ushairi huchangamana nayo.

Kwa mujibu wa maelezo ya wataalamu mbalimbali tuliyodurusu kuhusu dhana ya dhamira, tunaona kuwa kipengele hiki kimekuwa kichocheo katika kutuelekeza na kutuonesha njia ya kuzitalii na kuziiibua dhamira za Andanenga kutoka katika diwani zake.

### 2.3 Mapitio ya Kazi za Andanenga

Wataalamu kadha wameandika kazi zao kwa kuonesha maisha ya washairi na dhamira ya kazi zao za kisanaa. Hata hivyo, kazi hizi ni chache ukilinganisha uwepo wa uwingi wa washairi wenyewe na kazi zao.

Waandishi wachache wamejaribu kupitia kazi za Andanenga na kuonesha kuridhishwa kwao na mshairi huyu mwenye lakabu ya Sauti ya Kiza.

Pd. Leo Van Kessel (1993:7/2001:9), katika dibaji ya *Diwani ya Ustadh* na *Bahari ya Elimu ya Ushairi*, kwa ufupi sana, anamuelezea Andanenga kama kipofu anayeona wazi maana ya lugha kwani anatunga, anapamba na hata kughani mashairi ili kuwafurahisha na kuwafunza watu wengi. Katika dibaji yake, anamuelezea Andanenga kama mshairi bora kwa kutunga mitindo na miundo mingi ya ushairi wa Kiswahili na kufafanua utajiri wa Kiswahili ulio na aina nyingi kama samaki Baharini. Dibaji hii, inatupa ari na msukumo wa kutaka kujua kwa kina mengi kuhusu mshairi huyu ambaye ni mlemavu wa macho.

Naye Mayoka (1993:8-16) katika utangulizi wa *Diwani ya Ustadh*, anaamuelezea Andanenga kuwa si mshairi wa kupapasa. Ni mshairi bulibuli. Mayoka anamuelezea Andanenga kuwa ni mwandishi wa makala mbalimbali za lugha na ushairi wa Kiswhili magazetini. Kutokana na mapenzi yake ya lugha ya Kiswahil na ushairi, ndipo washairi na wanachama wa Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA) wakamchagua kuwa kiongozi katika chama ambacho alikitumikia katika ngazi kadha wa kadha. Katika utangilizi huo, Mayoka anaeleza kuwa; Andanenga amewahi kuwa mshiriki katika kipindi maarufu cha ***Ngano za Ushairi*** kilichokuwa kinatolewa na Idhaa ya Taifa ya Redio Tanzania, Dar es Salaam.

Umahiri wake unaonekana hadi sasa ingawa yu kipofu. Mayoka anamwona Andanenga kuwa ni mshairi mwenye utajiri mkubwa wa lugha na fani katika sanaa ya ushairi. Na mashairi yake yamejaa mafunzo na mawaidha kwa jamii. Mayoka anaeleza kuwa mshairi huyu anastahiki shumbe. Hata sasa katika kituo cha televisheni ya TBC, Andanenga anashiriki mjadala wa kipindi kiitwacho Ulimwengu wa Kiswahili.

Chamba (2011) alifanya utafiti katika kuangalia dhamira kwenye nyimbo za wasanii wasioona na mtazamo wao kwa jamii. Katika kazi yake, Chamba alijikita zaidi katika kuwaangalia wasanii wawili wenye ulemavu wa macho ambao ni Boniface Kiyenze ambaye ni kiongozi wa **The Seven Blind Band** na Mzee Abdallah Chembe ambaye ni kiongozi wa **The Ten Cultural Troup** akibainisha mchango wao wa kidhamira huku akimdondoa kwa ufupi Andanenga ambaye naye pia ana ulemavu wa macho. Akimtaja kama mshairi wa ngazi ya juu katika sanaa ya ushairi ambaye inafaa kufanyiwa utafiti wa kina. Dhamira nyingi zilizojitokeza na kujadiliwa katika nyimbo za wasanii hawa ni zile zinazohusu masuala ya haki na usawa kwa watu wenye ulemavu, rushwa, mapenzi na ndoa, ukimwi, uzalendo na unyanyapaa. Kwa mfano katika wimbo wa haki kwa watu wenye ulemavu wa **The Seven Blind Band** ***(uk.35)*** wanasema:

**Watu wenye ulemavu, haki zao wapewe**
**Watendewe mambo yote, watendewayo wengine**
**Pia wanayo haki, kushiriki maamuzi**
**Yawahusuyo wenyewe, na jamii kwa jumla.**

Alhaji Ally Hassan Mwinyi Rais mstaafu wa awamu ya pili wa Tanzania (2001:7-8) katika utangulizi wa *Bahari ya Elimu ya Ushairi,* anamuelezea Andanenga kuwa ni mshairi anayestahiki pongezi za dhati na shukrani kwa kutuelimisha kuhusu vipengele mbalimbali vya fani ya ushairi. Alhaji Mwinyi anatujuza kuwa,

Andanenga ameweza kubainisha miundo na mitindo tofauti ya mashairi kama vile uwili *(Mathna),* utatu *(Tathlitha),* unne *(Tarbiya),* utano *(Takhmisa)* na usita *(Sudusia).* Pia kitabu chake kinaeleza kanuni zinazotawala fani ya utunzi wa mashairi.

Katika utangulizi wake Mwinyi anaeleza kuwa, kitabu hiki kinatoa burudani na mafunzo. Anamaliza utangulizi wake kwa kusema kuwa: "Ingawa msanii Andanenga, kwa bahati mbaya, amepoteza nuru ya macho yake, lakini upungufu huo haukuzima nuru ya umahiri wake. Ni dhahiri kabisa kwamba kile kilichopungua katika macho kimefidiwa kwa ukamilifu katika akili. Ndio maana leo tunasoma utunzi wake. Ni kweli iliyoje kwamba *kuzima koleo siyo mwisho wa uhunzi*. Kama wahenga wasemavyo".

## 2.4 Hitimisho

Kwa kuhitimisha eneo hili, tumeweza kuona mapitio ya kazi mbalimbali za wahakiki, watafiti na wataalamu wachache mbalimbali wa Kiswahili kuhusu mashairi ya Andanenga ambazo ndiyo zenye mnasaba na mada yetu ya utafiti. Kazi za mapitio za wataalamu hawa zimekuwa dira kwa mtafiti katika kubaini mchango wa Andanenga katika ushairi wa Kiswahili kidhamira na kimuundo.

# SURA YA TATU

# MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti amejielekeza katika ubainishaji wa mkakati uliofuatwa katika mchakato wa kukusanya data, kuzichambua na hatimaye kuziwasilisha kwa ajili ya matokeo. Lakini pia sehemu hii inaonesha mpango mzima wa utafiti, eneo la kufanyia utafiti, mbinu za kukusanyia data na mawanda ya utafiti.

## 3.2 Uchambuzi wa Data

Utafiti huu ulitumia njia ya ufafanuzi iliyoongozwa na nadharia ya uhalisia na umuundo. Njia hii hutumika kuchambua data kupitia maelezo kwa kuwa utafiti huu ni wa kimaandishi ya kifasihi ambao data zake siyo za kinumerali. Hivyo, njia hii ndiyo iliyotumika katika utafiti huu.

## 3.3 Mbinu za Kukusanyia Data

Utafiti huu umetumia vyanzo vikuu vitatu vya kukusanyia data. Vyanzo hivyo ni: Maktabani, Uwandani na mahojiano ya mtu mmoja mmoja. Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data ni udurusu wa mapitio mbalimbali, maandiko ya kazi zinazomuhusu Andanenga na mahojiano. Ukusanyaji wa data uwandani umeendeshwa kwa kutumia mbinu ya hojaji, ili kuweza kubaini mchango wa mwandishi huyu katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili. Miongoni mwa watu waliohusishwa katika hojaji hizo ni pamoja na washairi, wahakiki wa Fasihi ya Kiswahili, wanaojishughulisha na utanzu wa ushairi pamoja na ndugu, jamaa na marafiki wanaomfahamu mwandishi huyu.

Vifaa vingine vilivyotumika katika hojaji ni, vinasa sauti na picha mgando. Vinasa sauti vimesaidia wakati wa uchambuzi wa data kwa kuwa si rahisi kuandika kila kitu wakati wa mahojiano. Picha mgando zitakuwa ithibati ya uhalali na ukweli wa data.

### 3.4 Mbinu za Kupata Sampuli

Mbinu ya sampuli lengwa ndiyo iliyotumika katika utafiti huu. Watu walihojiwa kutokana na uwelewa wao kuhusu mada husika. Uchaguzi wa mbinu hii unatokana na ukweli kwamba hii ni mada inayohitaji data kutoka kwa wataalamu wa fasihi na ushairi wa Kiswahili na si kwa kila mtu.

#### 3.4.1 Sampuli ya Watafitiwa

Sampuli ya utafiti huu ilichaguliwa kwa utaratibu ufuatao: kwanza, ni vitabu viwili vya mshairi huyu ambavyo vilitumika katika tasnifu hii. Vitabu hivyo ni pamoja na *Diwani ya Ustadh (1993)* na *Bahari ya Elimu ya Ushairi (2002).* Vitabu hivi vya mlengwa wa utafiti vimetusaidia katika kubaini mchango wa kimuundo na kidhamira wa mwandishi huyu. Kundi la pili ni la washairi wanne. Kundi la tatu ni la ndugu, jamaa na marafiki wa mwandishi ambao ni watano na mwisho ni mlengwa mwandishi mwenyewe. Hivyo basi sampuli ya watafitiwa katika utafiti huu ilikuwa na idadi ya wasailiwa kumi na mbili.

#### 3.4.2 Mahali pa Utafiti

Mahali pa utafiti huu palikuwa katika miji ya Dar es salaam, Dodoma na Morogoro. Sababu za uchaguzi wa maeneo hayo ni kuwa; Dar es salaam ndipo mahali ambapo mshairi huyu anapopatikana pamoja na ndugu na jamaa zake wengi, lakini pia ni mahali ambapo udurusu maktabani ulifanyika, hasa katika maktaba ya Taifa na

makavazi ya TATAKI ambapo maandiko mengi ya Fasihi ya Kiswhili na ushairi yamehifadhiwa. Morogoro ipo karibu na Dar es salaam, hapo yalifanyika mahojiano na baadhi ya washairi maarufu wa mji huo hasa wale wanaomjua. Dodoma ni mahali ambapo tumefanya mahojiano na baadhi ya washairi na kutumia maktaba ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

### 3.5 Nadharia za Utafiti

Nadharia ni istilahi ya kijumla inayomanisha miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya fasihi kuielewa kazi hiyo katika vipengele vyake vyote. Ni maelezo ya jambo lenye kufungamana na vigezo vilivyowekwa au vinavyoibuka kutokana na majaribio ya jambo hilo. Hii ina maana kwamba nadharia inaweza kutokana na mawazo yaliyoundwa kitambo na mtaaluma mmoja au jopo la wataalamu na inaweza kutokana na usomaji makini wa kazi ya fasihi au mtu binafsi (Todorov, 1977:13-14).

Katika kupambanua dhana ya nadharia, Mushengyezi (2003:1) anaandika:

> *"Nadharia huelezwa kama maarifa yaliyopangwa kwa usahihi ili kuelezea dhamira au wazo Fulani"* .

Kwa maoni ya mtafiti nadharia ni mpangilio wa mawazo yenye mantiki yenye kukusudia kufafanua ukweli fulani.

Katika utafiti huu, mtafiti aliongozwa na nadharia mbili yaani ile ya uhalisia na umuundo. Mtafiti ametumia nadharia hizi kwa sababu kazi yake ilijikita zaidi katika kuchambua fani na maudhui. Nadharia ya uhalisia imetumika katika kuchambua data upande wa maudhui hasa katika kipengele cha dhamira ambacho mtafiti ndicho alichokizamia katika utafiti huu na nadharia ya umuundo imetumika katika

kuchambua fani hasa katika kipengele cha muundo ambacho mtafiti amekitalii kwa undani.

Uhalisia ni hali ya ukweli kuhusu kitu au jambo na utayari wa kuupokea ukweli huo au kuutendea kwa njia inayowezekana. Ni mtindo wa sanaa na fasihi ambao hujaribu kuwasilisha jambo ambalo linafahamika au liko katika maisha halisi. Uhalisia wa kifasihi unaashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha ya kilimwengu na binadamu jinsi yalivyo.

Snow (1968:117) anaeleza kuwa nadharia ya uhalisia katika upana wake humaanisha uwakilishi wa uhalisia wa mambo katika fasihi. Nadharia hii ilizuka katika karne ya kumi na tisa nchini Ufaransa. Nadharia hii iliibuka ili kupinga nadharia ya ulimbwende ambayo ndiyo ilikuwa maarufu kipindi hicho. Nadharia hii ilianza kuonekana katika kazi za Jorge Luis Borger na kuendelezwa na Honors de Blazae nchini Ufaransa. Hatimaye nadharia ilienea sehemu nyingine ulimwenguni kutokana na kazi za wanafasihi mbalimbali. Nchini Uingereza kwa mfano nadharia hii iliingizwa na kazi ya Eliot na nchini Marekani iliingizwa na kazi ya Housell.

Katika kufafanua dhana ya uhalisia, Durey (1998:122-125) anaeleza kuwa, uhalisia unahusu uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu. Katika kitabu chake kinachoitwa *Aesthetic* (ujumi) mwanafalsafa Hegel alilitumia neno uhalisia kumaanisha kazi ya sanaa iliyo na wahusika ambao matendo yao wanayotenda yanachochewa na yanathibitishwa na hali ambayo wahusika hao wamo.

Naye Morris (2003:44) anasema kuwa nadharia ya uhalisia ilianza kuhusishwa katika fasihi kwa sababu waasisi wa nadharia hii waliona kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya kazi za sanaa na mtazamo wa msanii kuhusu mazingira aliyomo.

Dhana ya uhalisia ilianza kutumika kwa maana hii mpya kutokea takribani mnamo mwaka 1790. Emmanuel Kant katika chapisho lake lililoitwa *Critique of judgment (1928:98)* alitumia istilahi ya udhahania kama kinyume cha uhalisia. Kufikia mwaka 1798 wahakiki kama Schiller walikuwa wakitumia maneno haya yaani udhanifu na uhalisia kuashiria kinyume (Wellek, 1960:22-23).

Uhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa (Tallis, 1998:3-8). Mtazamo huu unatia mkazo kwenye uwasilishaji wa mambo ambayo yanaonekana katika jamii. Waandishi wanaoandika katika mkondo huu wanatarajiwa kutoa picha za wahusika, matukio na mandhari ambayo yanaoana kwa kiasi kikubwa na uhalisia wa jamii ya mwandishi anayehusika.

Uhalisia kama nadharia ya kiuhakiki ni mkondo unasisitiza usanii wa matukio katika fasihi ufanye matukio hayo yajitokeze kama yalivyo katika maisha ya kila siku na kuzingatia namna ukweli unavyosawiriwa katika nyakati na vipindi mbalimbali. Hivyo, nadharia ya uhalisia husimamia misingi na mihimili ifuatayo:

i. Msanii hujitahidi kuyachora maisha jinsi yalivyo bila kuathiriwa, na hufanya hivyo kupitia vipengele muhimu vya maisha kama vile siasa, uchumi, jamii, utamaduni na mapenzi.

ii. Lugha huwa ni ya kawaida, ikitumiwa na wahusika kama ilivyo katika maisha ya kila siku.

iii. Matukio huwa ni yale yanayoonekana, yanayojulikana au yanayowezekana. Hutarajiwa mambo hayo yaendane na jamii husika.

iv. Msanii huangalia matatizo ya jamii na kuchunguza chanzo chake. Huchunguza mabadiliko ya kihistoria ambayo husababisha hali mbalimbali za maisha, ikiwa ni pamoja na kuathiri mifumo ya fikra.

Aidha jambo la msingi lililomsukuma mtafiti kuteua nadharia ya uhalisia katika kuchanganua data zake kunatokana na ukweli kuwa mashairi mengi yaliyoandikwa na Andanenga yamejikita zaidi katika kuelezea na kujadili mambo halisi yanayomzunguka yaliyopo katika jamii yake kama vile siasa, uchumi, utamaduni na mapenzi. Hivyo, tunapotumia nadharia hii katika fasihi, tunataka kuona ni kwa kiasi gani mtunzi wa kazi ya fasihi anatuleta karibu na maisha ya kawaida ya kila siku.

Kutokana na maelezo hayo, kama nilivyoonesha huko nyuma nadharia ya uhalisia ndiyo iliyotumika katika utafiti huu katika kuchambua maudhui hasa katika kipengele cha dhamira ambacho ndicho tulichoshughulika nacho.

Umuundo ni nadharia ambayo mtafiti aliitumia katika uchambuzi wa fani katika utafiti huu. Msukumo wa kutumia nadharia hii unatokana na ukweli kuwa mtafiti alijikita katika kukizamia kipengele cha muundo katika kuangalia mchango wa Andanenga katika ushairi wa Kiswahili.

Umuundo ni nadharia iliyoanzishwa katika miaka ya 1960 na wataalamu Ferdinand de Saussure katika kitabu chake kinachojulikana *A Course in General Linguistics (1993:10-11)* na Roland Barthes katika kitabu chake kinachoitwa *Structuralism and Semiotics (1988:78).* Wote walijikita katika kuona kuwa fasihi hutoa maana kutokana na mpangilio wa vipengele kadhaa katika andiko.

Todorov (1977) naye anadahili kuwa, Umuundo hulenga na hujikita katika kuainisha sifa za kisanaa zinazopatikana katika fasihi kama taaluma inayojitegemea. Kwa mantiki hiyo ni wazi ushairi ukiainishwa kwa kutumia nadharia hii hasa katika upande wa fani, huainishwa na kuonesha mbinu zinazofanya utanzu huu kuwa na mvuto wa kishairi kama vile matumizi ya taswira, ishara, idadi ya mistari, vina na mizani na miundo mbalimbali ya ushairi.

Kutokana na maelezo ya Todorov, ni dhahiri kuwa nadharia ya umuundo ina mashiko ya kutosha katika uchambuzi na uhakiki wa fasihi hasa katika kipengele cha fani tunapoangalia ujenzi wa maumbo katika kazi ya fasihi.

### 3.6 Hitimisho

Kupitia nadharia hizi mbili za uhalisia na umuundo, ni dhahiri kuwa zilikuwa muongozo katika mkakati wa ukusanyaji na uchambuzi wa data katika kuwasilisha matokeo ya utafiti huu.

# SURA YA NNE

# UCHAMBUZI NA UCHANGANUZI WA DATA ZA UTAFITI


## 4.1 Utangulizi

Sura hii imejielekeza katika kuangalia mjadala ambao ni matokeo ya utafiti huu sambamba na malengo ya utafiti yaliyokusudiwa. Mjadala umegawanyika katika sehemu mbili ambazo zinatokana na maswali yaliyokuwa dira ya utafiti huu, yaani: kubainisha mchango wa dhamira katika ushairi wa Andanenga na kubaini mchango wa kimuundo katika ushairi wa msanii huyu katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili.

## 4.2 Maelezo kuhusu Vitabu Teule

### 4.2.1 *Diwani ya Ustadh*

*Diwani ya Ustadh* ni kitabu cha kwanza cha mwandishi Amiri Sudi Andanenga. Toleo la kwanza la kitabu hiki lilitoka mwaka 1993 na toleo la pili lilitoka mwaka 2001. Matoleo yote mawili ya kitabu hiki yamepigwa chapa na kampuni ya Benedictine Publications Ndanda – Peramiho Tanzania. Diwani hii ina jumla ya mashairi sabini na nne yanayojadili masuala mbalimbali ya kiuchmi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Mashairi mengi katika Diwani hii yanajadili zaidi masuala ya Uzalendo, Kuhusu Kiswahili, Kuusemea Ushairi, Kulumbana, Mapenzi, Majonzi na Kuombeana Heri, pamoja na Rai na Mawaidha. Ni diwani iliyosheheni mafunzo na mawaidha kwa jamii.





**Kilelezo Na 9: Jalada la Diwani ya Ustadh (1993) Chanzo: Data za utafiti (2014).**

Hakika Diwani hii imedhihirisha dhahiri kuwa Andanenga ni Ustadh. Ustadh ni neno la Kiarabu lenye maana ya mwalimu katika lugha ya Kiswahili. Hivyo, katika kitabu hiki mwandishi ameonesha wazi kuwa yeye ni mwalimu kwa kuweza kutufunza mambo mbalimbali yaliyomo ndani ya jamii. Kadhalika, kitabu hiki kimesheheni miundo na mitindo mbalimbali ya ushairi wa Kiswahili lakini pia utanashati na ufundi wa lugha katika diwani ya Ustadh ni wa kuvutia.

### 4.2.2 Bahari ya Elimu ya Ushairi

Katika utangulizi wa kitabu hiki, Rais mstaafu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Alhaji Ali Hassan Mwinyi alisema: *"Jina la kitabu hiki* ***Bahari ya Elimu ya Ushairi,*** *limesibu sana. Kwani maudhui yake yana muafaka na jina lenyewe. Ni kweli fani ya ushairi ni pana, tena ina kina kirefu kama bahari yenyewe".*




**Kilelezo Na 10. Jalada la Diwani ya Bahari ya Elimu ya ushairi (2002): Chanzo: Data za utafiti. (2014)**

Kwa vile bahari ndimo hupatikana aina zote za samaki, humu pia mwafanana, kwani aina ya mitindo, maumbo na miundo anuai ya ushairi inaweza kuvuliwa toka bahari hii kuu. Kwa maneno yake Andanenga *Uk. 13* mwandishi wa diwani hii anatumia jazanda na anatongoa hivi;

**Ushairi ni Bahari, vititini tuzamie**
**Nyangumi na sansuri, na chewa tujivulie**
**Tukavue majodari, na changu tukajilie**
**Vilindi tuvifikie, lulu tukajipatie.**

**Twendeni kwa kubwa ari, kamwe tusipuuzie**
**Twendeni tusisubiri, uvivu tusijitie**
**Hima wenye manowari, na wa meli tuingie**
**Mavuvi tukusudie, ukwasi utuingie.**

Diwani hii inabainisha fani mbalimbali za sanaa ya ushairi; kuanzia mashairi ya kawaida hadi tenzi, nyimbo za tarabu, nyimbo za maombolezo na kadhalika. Pia diwani imebainisha miundo tofauti ya mashairi kama vile uwili *(Mathna),* utatu *(tathlitha),* unne *(tarbiya),* utano *(takhmisa)* na usita *(sudusia).* Pia diwani hii inaelezea miundo, mitindo na kanuni zinazotawala fani ya utunzi wa mashairi. Aidha Kitabu hiki kinatarajiwa kuwa ni cha manufaa makubwa kwa kila apataye bahati ya kukisoma. Kinatoa burudani na mafunzo kwa akisomaye.

### 4.3 Mchango wa Kidhamira wa Andanenga katika Ushairi wa Kiswahili

Katika ushairi wa Andanenga kuna dhamira nyingi zinazojitokeza. Katika vitabu teule ambavyo ni chanzo cha utafiti huu mwandishi ameweza kujadili mambo mengi yaliyomo katika jamii, mambo ambayo yakijitokeza zaidi katika nyanja za uchumi, siasa, na utamaduni.

Kwenye kitabu cha *Diwani ya Ustadh* kuna dhamira nyingi zilizojitokeza. Kuna swala la uzalendo kama lilivyojadiliwa katika shairi la ***Mvunja Kwao (uk. 17-18).*** Katika shairi hili, mwandishi anawaona watu wasiothamini kwao kuwa ni majura na waliopotea na hawana akili timamu. Katika ubeti wa kumi na tatu wa shairi hili, mwandishi anasema:

**Mvunja kwao fedhuli, wala hana njema dira**
**Atakapo kuwa mbali, muwinde mfunge nira**
**Akwombapo usijali, mvute kama kachira**
**Mvunja kwao ni jura, mradi hana thamani.**

Maudhui ya shairi hili yanahalisika kabisa. Kwani kuna baadhi ya wanajamii hukosa uzalendo na kudharau kwao na kuona kwamba sehemu nyingine ambazo si za kwao ni bora. Kwa mfano wapo baadhi ya wanajamii leo hii hususan vijana wao huona nchi za magharibi na tamaduni zao ni bora kuliko za kwao. Hivyo, tabia hii huwafanya vijana wengi kudharau kwao. Tena wengine huenda mbali zaidi kwa kudai kuwa ni heri uzaliwe mbwa Ulaya kuliko binadamu Afrika.

Fauka ya hayo, katika *Diwani ya Ustadh*, mwandishi pia amezungumzia suala la pendo lenye kutaka pesa, akitumia shairi la ***Pendo la pesa (uk. 91)*.** Katika kujadili dhamira hii, Andanenga anaonekana kukerwa sana na aina hii ya pendo ambalo linajali sana pesa kuliko utu na upendo wa dhati. Mwandishi anasema kuwa, pendo la pesa si pendo na kamwe huwa halina utamu na limejaa uvundo. Mwandishi anaiasa jamii kuachana na aina hii ya pendo kwani pendo la dhati na la kweli huwa halijali pesa, dini wala kabila. Katika ubeti wa tano wa shairi hili mwandishi anasema:

**Pendo kutumia hela, mifuko iteketee**
**Pendo hilo lahaula, ni zigo ujibebee**
**Pendo wawili ni kula, nyama ndimi mnenee**
**Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo.**

Kimsingi dhamira ya shairi hili inahalisika kwa kiasi kikubwa katika jamii. Hii inatokana na ukweli kuwa mapenzi siku hizi kwa kiasi kikubwa yanajali zaidi pesa kuliko kitu kingine. Hali hii imepelekea mapenzi kuwa bidhaa kama zilivyo bidhaa nyingine zinazouzwa sokoni na madukani. Hii inatokana na mfumo wa kibepari na mabaidliko ya wakati na mazingira ambapo pesa imekuwa ndiyo msingi wa kila kitu.

Leo imebainika kuwa wanawake wanauza miili yao kama bidhaa kwa lengo la kujipatia pesa na mahitaji mengine.

Suala la mapenzi pia limejadiliwa ndani ya *Diwani ya Ustadh*. Katika shairi la ***Fanya ulizio (uk. 89)*** Andanenga anayaona mapenzi hutoa utulivu, dawa na huwa na ladha. Mwandishi anatueleza kuwa mapenzi hayataki bughudha wala adha kwani mapenzi ni dawa ya watu wawili walio wagonjwa na tiba yao ni penzi la dhati baina yao. Mtunzi anaishauri jamii kuwa penzi la dhati hupewa mmoja na siyo wengi hivyo anawaonya wale wenye tabia hizo kubadili tabia. Katika ubeti wa kwanza, tatu na nne mwandishi anasema:

**Leo nina jambo, nataka kwambia**
**Sikiza mrembo, badili tabia**
**Mapenzi ya shombo, sitavumilia**
**Nataka mapambo, sitaki udhia.**

**Mapenzi ni dawa, ya watu wawili**
**Wagonjwa hupowa, wakawa sahali**
**Wakavuta hewa, hata ilo mbali**
**Kama hujajuwa, kaa ujadili.**

**Na wala si haja, wengi kuambata**
**Mmoja ni tija, ni huyo limbata**
**Lumbata mmoja, pendo la mashata**
**Pendo la faraja, liwe la kumeta.**

Pamoja na mawazo ya mwandishi, hali halisi katika jamii ya sasa, imefanya mapenzi ya dhati kuwa nadra sana. Watu wamejikita katika kupenda kwa kuangalia hali ya uwezo na umaarufu wa mtu.

Katika *Bahari ya Elimu ya Ushairi,* mwandishi pia amejadili suala la mapenzi. Lakini ni mapenzi ya kupenda macho. Akitumia shairi la ***Macho yako (uk. 32)***, Andanenga anaonekana akisifu uzuri wa macho ya mpenzi wake. Macho ambayo

yanamfanya ashindwe kuficha mapenzi yake ya dhati kwa mwenziye. Kwa maneno yake katika shairi hilo lenye beti moja tu mwandishi anasema:

**Nayapenda macho yako, pindi ukiyafunua**
**Kwa hakika mboni zako, kwa mwanga zamemetua**
**Ndipo kwa haiba kwako, nashindwa kujitambua**
**Najihisi nimetua, katika penzi la kua.**

Andanenga anaiasa jamii kuwa na mapenzi ya dhati na siyo ya chati. Mapenzi ya dhati ni jambo muhimu sana katika maisha ya mwanadamu. Kwani husaidia kuepusha maradhi, fitina, migogoro na hata mauaji katika jamii. Lakini pia mwandishi anahamasisha jamii iwe na desturi ya kusifu uzuri na urembo wa wapenzi wahusika kwani jambo hili huongeza huba na mawada kwa wapendanao.

Dhamira nyingine iliyojitokeza katika *Diwani ya Ustadh* ni swala la wema. Mwandishi anaeleza kuwa wema ni jambo muhimu sana katika maisha ya kila siku ya mwanadamu na waumini wao huona kuwa ni agizo kutoka kwa Mola. Lakini leo hii binadamu wamekosa chembe ya wema na wamekuwa makatili na madhalimu. Katika shairi la ***Wema (uk 82)*** ubeti wa tano na wa nane twamwona mwandishi anasema:

**Wema kwa mola agizo, soma katika miraji**
**Tufanye bila legezo, kesho tupate mtaji**
**Wema bila bembelezo, kaagiza muumbaji**
**Wema ni kitu buruji, popote ni muangazo.**

**Wema huwa darahamu, ukipata uleaji**
**Wema huwa na shahamu, ukikosa ufujaji**
**Wema hautatehemu, ukipata watendaji**
**Wema ni kitu buruji, popote ni muangazo.**

Beti hizi zinaweka wazi jinsi gani mwandishi anvyouona wema kuwa ni kito cha thamani pale anaposema ni mwangaza katika kuangazia mambo mbalimbali. Mwandishi anaiasa jamii kuwa kamwe isije kuufuja wema, na malipo ya wema yana mtaji mkubwa kwa mungu.

Katika *Diwani ya Ustadh,* dhamira ya dini nayo imejitokeza katika shairi la ***Dini (uk. 87).*** Mwandishi anatueleza kuwa dini ndicho kitu kinachomuongza mwanadamu kuwa karibu na Mungu wake. Katika ubeti wa tano na sita mwandishi anadondoa hivi:

**Dini zipewe heshima, zisipalazwe kinaya**
**Kitakiwacho kusoma, ujuwe wapi kwapwaya**
**Siyo ovyo kuloloma, ja magari yenda Mbeya**
**Dini ajali kifaya, faradhi zake Rabiya.**

**Tuwe watu watulivu, tupatwe na njema ruya**
**Siyo kuleta ukavu, magomvi na nyingi maya**
**Maovu na ukatavu, vyapingwa kwenye hikaya**
**Dini ajali kifaya, faradhi zake Rabiya.**

Katika shairi hili, mwandishi amedhamiria kuiasa jamii kuheshimu dini ya kila imani na ametaka vitabu vya dini visomwe na vieleweke. Mwandishi anaitaka jamii kuwa tulivu na kuepusha ugomvi na migogoro ya kidini, kwani dini zote zinakataza na kukemea vikali maovu ya aina yeyote. Kimsingi, dhamira hii inasadifu mazingira halisi ya jamii.  Kwa sasa, dunia imechafuka kwa migogoro ya udini. Kwa mfano nchini Nigeria na Jamuhuri ya Afrika ya Kati watu wanabaguana na kuuana kwa sababu ya tofauti ya kidini. Kadhalika Tanzania, nayo hali yake si shwari baadhi ya watu wamepandikizwa chuki za udini na wanasiasa makanjanja ambao hawaitakii kheri Tanzania. Kumekuwa na matukio ya mauaji na kumwagia tindi kali viongozi wa dini pamoja na uchomaji moto wa nyumba za ibada.

Katika *Bahari ya Elimu ya Ushairi,* dhamira ya dini imejitokeza katika shairi la ***Toba (uk. 32).*** Katika shairi hili mwandishai anahimza watu kuomba toba na kumkurubia Mungu. Mwandishi anatueleza kuwa toba ni kitu cha lazima kwa mwanadamu katika kumtubia mola wake ili aweze kuingia peponi na kupata salama ya kesho akhera. Katika ubeti wa kwanza wa shairi hilo, mwandishi anaandika:

**Toba kwetu ni lazima, kwake mungu tutubie,**
**Kesho nyumba ya salama, kwa shangwe tukaingie**
**Shukrani zote njema, zake muumba wa sie**
**Tumwae zimfikie, swalatu wa tasilima.**

Mwandishi katika shairi hilo anaiasa jamii kuona kuwa maisha ya duniani yana mwisho, hivyo yafaa kufanya ibada na toba na kujikurubisha kwa muumba na kumtegemea yeye kwa kila kitu. Mshairi anaona yafaa wanajamii kuishi kwa kufuata misingi na matakwa ya Muumba wa dunia.

Katika *Diwani ya Ustadh*, dhamira ya rai na mawaidha ya dini imejadiliwa katika shairi la ***Wosia (uk. 83).*** Katika shairi hili mwandishi anaonekana kumuasa kijana wake wa kiume aitwaye Sudi juu ya mambo mbalimbali ya kidunia. Mtunzi anamuasa kijana wake kuacha tabia ya kunusa na kugusa vitu vya watu. Bila ya shaka hapa anamuasa kijana wake aache umbeya na wizi na hivyo apingane na tamaa yake. Aishi vema na watu na kumkataza kuambatana na watu wenye tabia mbaya kwani wanaweza kumletea matatizo. Pamoja na hayo mwandishi anamuasa kijana wake kuiogopa sana dunia na kumtaka ajitenge na masahibu yake. Asipofata mwendo mwema na uadilifu, vyombo vya sheria vitamweka ndani. Ubeti wa ishirini na sita na wa thelethini na moja zote zinasema hivi:

**Vya watu kunusanusa, liogope jambo hilo**
**Kunusa au kugusa, baya sana tamanilo**
**Wewe huenda kunasa, likakoswa litegwalo**
**Ufichwe penye totolo, usione nyumba mbele.**

**Nakufunda kwa busara, ukae vema na watu**
**Kesho ukenda akhera, kila swali utafutu**
**Ufutu yasiyo dhara, yenye mwanga metumetu**
**Uwazidi mara tatu, kwa wema wataochuma.**

Ndani ya *Bahari ya Elimu ya Ushairi*, mwandishi anatoa rai na mawaidha kwa kuiasa jamii kutenda yaliyo mema hapa duniani. Katika shairi la ***Tutende Mema (uk. 53),*** mwandishi anaeleza kuwa usihadaike na umri wa hapa duniani ambao unao mwisho wake. Daima utende mema kabla ya siku ya hukumu. Tamaa ya nafsi iache. Ubeti wa tatu wa shairi hili unasema:

**Usihadaike, umri ulio na mwisho**
**Mema yaandae, wende nayo kwa mola kesho**
**Mbele ya moliwa, ufike kwa matayarisho**
**Tamaa ya moyo, itakalo ipe kanusho**
**Siku ya hukumu, jahimu itakuepuka.**

Mshairi Andanenga pia amejadili dhamira ya umbea katika *Diwani ya Ustadh.* Mwandishi anaeleza kuwa umbea siyo kitu kizuri kwa mtu kukiendekeza. Kuwepo ndani ya jamii huaribu mambo mengi na husababisha ugomvi na chuki. Katika shairi la ***Umbea (uk.74),*** mwandishi anatuasa kuacha tabia ya umbea na kujitenga nao kwani hata katika maandiko matakatifu jambo hili limekemewa na kukatazwa vikali. Katika ubeti wa pili na tano, anadondoa:

**Umbea unaharibu, umbea si kupendeza**
**Umbea si mahisabu, umbea katu kujaza**
**Umbea ni majisibu, umbea unapunguza**
**Si kitu cha kupendeza, umbea unaharibu.**

**Umbea kwenye vitabu, umbea umekataza**
**Umbea Bwana wahabu, umbea hakuongoza**
**Umbea ukijaribu, umbea takuunguza**
**Si kitu cha kupendeza, umbea unaharibu.**

Kimsingi dhamira hii inasadifu mazingira halisi ya jamii zetu. Jamii zetu nyingi zimekuwa zikitumia muda mwingi katika kufanya umbea na kusababisha migogoro mingi na pia kutoelewana.

Katika *Diwani ya Ustadh* kuna swala la haki ya kupiga kura. Kura ni haki ya msingi na ya kikatiba kwa raia yeyote yule nchini. Kwa kutumia haki ya kura mabadiliko ya ungozi hutokea katika jamii. Mtunzi katika shairi lake la ***Haki ya Kupiga Kura (uk. 18)*** anaitaka na kuihimiza jamii kuona umuhimu wa kupiga kura na wala wasipuuze jambo hilo pale chaguzi mbalimbali za kitaifa zinapofanyika. Mwandishi anafafanua kuwa kura ni haki ya msingi ya kila raia na husaidia kuchagua na kupata viongozi wanaohitajika na walio waadilifu. Zaidi mwandishi anahimiza kuchagua viongozi walio wachapakazi, wenye bidii na makini. Wasichaguliwe kwa utamu wa maneno yao ya jukwaani au mavazi yao mazuri. Katika ubeti wa nne wa shairi hili, mshairi anasema:

**Tuchague viongozi, walo na njema tabia**
**Siyo kwa mema mavazi, nguo safi kuvalia**
**Twataka watekelezi, wenye bidii kutia**
**Tusipuuze raia, haki ya kupiga kura.**

Wananchi wengine hawaoni thamani ya kupiga kura katika kuchagua viongozi wao. Baadhi yao wamekuwa hawajitokezi katika zoezi hili muhimu. Wananchi wengine

wamekuwa mahiri katika kulaumu viongozi wao, pasi na kuangalia wao wenyewe huwa kwa kiasi gani walishiriki katika kuhakikisha wanapata viongozi bora.

Katika kitabu cha *Bahari ya Elimu ya Ushairi*, mwandishi hakuchelea kuifunda jamii kuhusu kuachana na matendo maovu yanayomchukiza Mungu na ambayo hayana manufaa katika ustawi wa jamii. Akitumia shairi la ***Jiepushe (uk. 84-85),*** mwandishi Amiri Sudi Andanenga anaikataza jamii kwa kujiepusha na haraka, uwongo, fitina, vitimbi na usaliti. Mtunzi anayoona matendo hayo yote kuwa ni ya kiovu na ya kishetani na hayastahiki kuwepo ndani ya jamii. Ubeti wake wa pili na wa nne wa shairi anasema:

**Jiepushe na haraka, haraka ni ya shetani**
**Kamwe haina Baraka, subira iyambateni.**

**Jiepusha na fitina, kwa mbali na majirani**
**Ufitina ni laana, machukizo kwa manani.**

*Diwani ya Ustadh*, imeibua dhamira ya utamaduni ambayo imejadiliwa katika shairi la ***Tusifu Utamaduni (uk. 20-21).*** Katika shairi hili mwandishi anahimiza kusifu utamaduni wetu na kuacha kasumba za kupenda na kusifu tamaduni za nje. Mwandishi anaihimiza jamii kupenda ngoma zake, lugha yake, pamoja na mila na desturi za Kiafrika. Mwandishi anakemea vikali tabia ya baadhi ya Waafrika kukumbatia na kuabudu mila na tamaduni za nchi za Magharibi na kuzibeza kwa kudharau mila na tamaduni za Kiafrika. Andenenga anasisitiza zaidi kwa kusema ni vyema kuonesha utamaduni wetu hadharani, kuufunza mashuleni na kuutangaza redioni ili uweze kurithisha amali za utamaduni kwa vizazi vijavyo. Katika ubeti wa tano na saba wa shairi hili mwandishi anaasa:

**Tusifu kwa kuonyesha, bayana na hadharani**
**Tufungue zetu kasha, tuone vilivyo ndani**
**Kwani inafurahisha tunapoona machoni**
**Tusifu utamaduni, wetu wa Kiafrika.**

**Tusifu kwa kuuremba, na kufunza mashuleni**
**Na midomoni kuimba, na huko maredioni**
**Mila zetu kuzipamba, ni fahari si huzuni**
**Tusifu utamaduni wetu wa Kiafrika.**

Andanenga anashauri umuhimu wa kupenda na kuenzi tamaduni na kuacha kuiga mila na tamaduni za Ulaya. Umekuwa ni mtindo kwa vijana katika jamii kupenda kujinasibu kwa lugha, nyimbo, miziki na hata mavazi ya kigeni.

Katika kitabu cha *Bahari ya Elimu ya Ushairi,* Andanenga amejadli swala la kuwaheshimu wazazi. Akitumia shairi la ***Heshima kwa Wazazi (uk. 84)*** na shairi la ***Wazazi (uk. 140-141)*** mwandishi anaeleza umuhimu wa kuwatendea wema wazazi kama shukrani kwa malezi na upendo waliotenda tulipokuwa wadogo. Wazazi hutumia muda wao mwingi katika kuhakikisha watoto wao wanaishi na kukua katika mazingira salama ya kimaadili. Wao uhakikisha wanawapa watoto wao elimu, chakula na mavazi. Aidha uhakikisha kuwa kila wanapoumwa uwapatia tiba. Mwandishi anabainisha kuwa hatuna cha kuwalipa wazazi kwa mema waliyoyafanya zaidi ya kuwatendea mema na kuwaonea huruma na kuwaheshimu wazazi wawili, Baba na Mama. Katika ubeti wa tatu wa shairi la ***Heshima kwa Wazazi,*** mshairi anahoji kwa kutoa changamoto kwa kusema:

**Nini tulipe, yalingane, yao matendo**
**Mema tuwape, si kingine, chenye muundo**
**Yangu meupe, tushikane, kwenye upendo.**

Na katika ubeti wa sita wa shairi la ***Wazazi*** mwandishi anadahili hivi:

**Kama tumepata mali, wao hali zimekwama**
**Mikono yetu miwili, tuwashikilie vema**
**Tusiwaache dhalili, watoto twanemanema**
**Tupende Baba na Mama, wazazi wetu wawili.**

Mwandishi katika dhamira hii anashauri kuwafanyia wema wazazi wawili kwani ndilo jambo pekee la kuwafariji na kuwaenzi wazazi kwa muda wao mwingi waliotumia katika malezi. Wapo baadhi ya vijana ambao hawana mapenzi na wazazi wao. Wao hawaheshimu, wala kuwasaidia bali huwaacha wakidhalilika na kunyanyasika.

Fauka ya hayo, katika *Diwani ya Ustadh,* mwandishi amejadili swala zima la uchumi. Kama ilivyo uchumi ndiyo nyenzo ya kuleta tija na maendeleo ya Taifa lolote lile ulimwenguni. Mataifa mengi makubwa na madogo hufanya jitihadi na kuanzisha mipango kadha wa kadha kwa lengo la kuinua uchumi wa nchi zao. Akitumia shairi la ***Uchumi (uk. 24),*** mwandishi anafafanua kuwa ili uchumi wa nchi uweze kuwa imara basi ni lazima ujikite katika kuimarisha viwanda, biashara na kilimo cha kisasa. Uthabiti ukiwekwa katika maeneo hayo basi uchumi utasimama na kuimarika. Katika ubeti wa kwanza wa pili na wa sita wa shairi, Andanenga anasema:

**Uchumi tunaposema, neno hili kila mara**
**Maana yake huduma, ziletazo itijara**
**Katika nchi nzima, toka Pwani hadi Bara**
**Uchumi ni biashara, viwanda na ukulima.**

**Viwanda na ukulima, na tatu ni biashara**
**Haya mambo ni daima, ni cha uchumi kinara**
**Kinara cha kuugema, uchumi wenye busara**
**Uchumi ni biashara, viwanda na ukulima.**

**Wananchi ni lazima, tukitaka tuwe bora**
**Ni lazima kujituma, kwa kusimama imara**
**Wa visiwa na mrima, kwa kazi si kuzurura.**
**Uchumi ni biashara, viwanda na ukulima.**

Mwandishi anatuweka hadhiri kuwa ili mambo yote hayo yaweze kuenda sawa ni lazima wananchi tujitume na kufanya kazi kwa bidii na tuache kulalamika, kuzurura mitaani na kupiga soga katika vijiwe na maskani. Dhana inayotiliwa mkazo hapa na mshairi ni kuwa, uchumi hausimami pasi na kuwa na ari ya kuchapakazi na kiunzi cha kujituma na kujibidiisha katika kila tendo.

Dhamira ya ushirika nayo imejitokeza ndani ya Diwani *ya Ustadh*, pale mwandishi alipotumia shairi la ***Ushirika (uk. 33).*** Yeye anaona kuna umuhimu wa watu katika jamii kushirikiana katika kuleta tija na maendeleo ya taifa. Mwandishi anaeleza kuwa ushirika ni jambo muhimu na la msingi sana katika kukuza uchumi wa nchi, hivyo anahimiza watu wajiunge katika vyama vya ushirika kwa lengo la kuinua vipato vyao. Katika ubeti wa saba na wa nane, mshairi anashauri:

**Ushirika kitu chema, aidha kina thamani**
**Thamani kwa sisi umma, na uchumi kwa nchini**
**Na tujiunge mapema, kitu kukawa acheni**
**Tuwemo ushirikani, tuupinge unyonyaji.**

**Tamati beti ya nane, ningali nawaiteni**
**Kwa pamoja tuungane, tuwemo ushirikani**
**Kusudi letu tuvune, tuondoke ufukweni**
**Tuwemo ushirikani, tuupinge unyonyaji.**

Mwandishi hapa anasisitiza kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Hili linathibitika katika mazingira halisi ya jamii yetu ya Kitanzania na hata ulimwenguni. Mataifa mengi leo hii yanafanya jitihada za makusudi katika kuunda ushirikiano wa kimataifa katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, kisiasa, kibiashara na kiusalama. Leo tunaona nchi za Afrika Mashariki zimo katika shirikisho la pamoja katika kuyaimarisha maendeleo ya nchi wanachama kimaendeleo. Yapo mashirika ya kikanda kama SADC, AU, UAE, EAC na EU ambayo yameanzishwa kwa azma ya  ushirikiano katika kuleta maendeleo yao. Nchini Tanzania kuna vyama mbalimbali vya ushirika vilivyoanzishwa tangu wakati wa awamu ya kwanza ya Uraisi wa Mwalimu Nyerere. Vyama hivi ni vile vyama vya ushirika vya wakulima na wafugaji na ushirika wa kuweka na kukopa kwa lengo la kuwafanya wananchi wawe na nguvu ya pamoja katika maswala mbambali ya kiuchumi na kijamii.

Ndani ya diwani ya Bahari *ya Elimu ya Ushairi*, mshairi amejadili swala zima la kuwa na tabia njema akitumia shairi la ***Tabia (uk. 159-160).*** Mwandishi anatueleza kuwa tabia njema siku zote huanza nyumbani kwa Baba na Mama, kabla ya hata ya watoto hawakwenda shuleni ambapo huko hukutana na walimu ambao nao pia husaidia kuwajenga watoto kimwili na kimaadili. Mshairi Andanenga anesema kuwa tabia njema ina thamani kubwa katika jamii kwani huondoa ugomvi na watu kuwa

furahani kwa muda wote. Lakini pia Andanenga anatukumbusha ule usemi kuwa *"tabia mbaya ni sifa ya shetani"* na mara zote huwa ina mavuno mabaya katika jamii. Katika ubeti wa pili na wa saba wa shairi tunaambiwa:

**Tabia njema huanza, Baba na mama nyumbani**
**Kwa watoto kuwafunza, kabla ya kwenda shuleni**
**Kusiwe wa kuyakinza, naomba tafadhalini**
**Tabia yenye thamani, ni yenye mwenendo mwema.**

**Tabia iso na haya, rafikiyo ni shetani**
**Kuisaliti himaya, na wenzi haupatani**
**Mavuno yako mabaya, kwa watu kukulaani**
**Tabia yenye thamani, ni yenye mwenendo mwema.**

Dhamira hii inasadifu mazingira halisi ya jamii, kwa sababu baadhi ya wazazi hushindwa kujenga misingi imara ya tabia njema kwa watoto wao, hivyo kuwapelekea vijana wengi kukosa adabu na heshima na wakati mwingine husababisha mzigo mkubwa kwa walimu pindi watoto hao wanapokuwa shuleni.

Ndani ya *Diwani ya Ustadh*, humo mwandishi amejadili swala la ujamaa. Akitumia shairi la ***Ujamaa (uk. 35),*** mshairi huyu anauona ujamaa ni mfumo ulio johari katika maisha ya wanadamu. Lakini mshairi hakusita kuonesha masikitiko yake, kwani baada ya kuona mfumo wa ujamaa katika utekelezaji wake umekuwa duni na unapigwa vita na mataifa makubwa ya mgharibi ambayo yanajinasibu kwa kuikuza falsafa ya kibepari. Katika ubeti wa kwanza wa shairi hili mtunzi anadadavua hivi:

**Ujamaa uhiwani, kitu kinachovutia**
**Hapa petu duniani, na kule tukiingia**
**Bali umekuwa duni, macho tunaufumbia**
**Tendo si kusimulia, wasifu wa ujamaa.**

Andanenga anauona ubepari kuwa ni kikwazo kikubwa katika ustawi wa maisha ya watu masikini, kwani ni mfumo usiozingatia usawa na wa kinyonyaji. Hivyo, anawashauri wanajamii kuishi kijamaa zaidi.

Katika *Diwani ya Ustadh,* mshairi amejadili sana suala la ushairi. Mtunzi anaonekena kufanya bidii kubwa katika kuuhami na kuutetea ushairi wa Kiswahili kwa kutunga mashairi anuai yenye kuutetea ushairi wa Kiswahili, kuwasifu washairi na pia kuwakemea wale wanaonekana kutaka kuudhoofisha ushairi wa Kiswahili. Akitumia shairi la ***Ushairi (uk. 46)*** mwandishi anawahimiza magwiji wote wa ushairi wa Kiswahili kuhakikisha wanafanya jitihada za kuuhami ushairi wa Kiswahili ili usije kupotoshwa na watu ambao hawana weledi wa taaluma hii. Mshairi anaona fani hii imeingiliwa na watu wajinga wanaotaka kuiua sanaa hii ya asili ya jadi. Katika ubeti wa pili wa shairi hili msanii huyu anasema:

**Kuuhami ushairi, washairi yatubidi**
**Washaingia mathori, wajinadio weledi**
**Kwa kupotoa nadhari, sanaa yetu ya jadi**
**Washairi yatubidi, kuuhami ushari.**

Sambamba na hili, katika kuonesha kuwa Andanenga ana mapenzi makubwa na ushairi wa Kiswahili, hakusita kuwasifu wataalamu na magwiji mbalimbali wa ushairi wa Kiswahili kwa tungo zao bora na zenye mchango mkubwa katika kufunza na kueleimisha jamii. Pia katika kuuendeleza ushairi wa Kiswahili. Haya tunayapata katika shairi la ***Tungo Zenu (uk. 48)*** ambapo ubeti wa kwanza, wa pili, na wa nne mwandishi, anaelezea hivi:

**Leo nashika kalamu, makusudi niandike**
**Nasifu wataalamu, ili mbali wajulike**
**Na kiongozi rahimu, fanya dhamiri itoke**
**Mkwawa na Mtu- Chake, tungo zenu zaridhisha.**

**Mtu-Chake na Mkwawa, nyie watunzi stadi**
**Kanuni mwazielewa hakuna wa kukaidi**
**Na ndipo sikuchelewa, kuwasifia abadi**
**Mrisho na Juma Sudi, tungo zenu zaridhisha**.

**Nyamaume, Hamduni, ninyi watunzi farisi**
**Mnatunga kama nini, sikuweza kukihisi**
**Ninawalia yamini, mumeshinda na kupasi**
**Dii Kei, Mathiasi, tungo zenu zaridhisha.**

Mwandishi anawataja washairi maarufu katika uga wa ushairi wa Kiswahili wa enzi zake kama vile; Mkwawa, Mtu-Chake, Juma Sudi, Nyamaume, Dii kei, Mnyampala, Bushiri, Kuyela, Chief Jaji, Kobakusha, Mwanahewa, Sihiyana na Kilunga. Hawa wote walikuwa washairi mahiri kwa wakati wake mwandishi. Baadhi ya washairi hao wameshatangulia mbele ya haki na baadhi yao wangali hai.

Kwa upande mwingine, katika *Diwani ya Ustadh,* mwandishi amejadili swala la lugha ya Kiswahili. Katika kujadili dhamira hii mwandishi anadhihirisha mapenzi ya dhati aliyonayo katika lugha hii. Mwandishi Andanenga akitumia mashairi kama vile; ***Kitangazwe Kiswahili (uk. 38), Kiswahili Mama (uk. 39)*** na ***Kiswahili Tukipambe (uk. 41),*** anaonesha ni kwa jinsi gani anavyoithamini lugha ya Kiswahili kwa kuisifu na kuitetea. Mathalani katika shairi la ***Kitangazwe Kiswahili (uk. 38),*** mwandishi anaiasa jamii katika kuitangaza lugha ya Kiswahili na kuacha kasumba ya kukikumbatia Kiingereza. Mwandishi anasikitishwa na jamii ya baadhi ya Watanzania ambayo inaiviza na kuvunja mihimili ya lugha ya Kiswahili na kuitukuza lugha ya Kiingereza. Hivyo basi, anaiasa jamii kuipa hadhi lugha ya Kiswahili na kuachana na lugha ya Kiingereza. Katika ubeti wa tatu wa shairi hili, mshairi anasema kwa lugha ya ukali:

**Kiswahili mwakiviza, mwakivunja mihimili**
**Chini kukigaragaza, mwakitia uthakili**
**Acheni kukichakaza, kukitia mushikeli**
**Juu kiwe Kiswahili, chini kiwe kingereza.**

Maudhui ya shairi hili yanasadifu mazingira halisi tuliyonayo nchini. Sehemu ya jamii ya Watanzania inathamini sana lugha ya Kiingereza kuliko lugha ya Kiswahili.

Hali hii imepelekea baadhi ya wanajamii kusadiki kuwa mtu anayezungumza Kiingereza ndiye msomi, hivyo huwapeleka watoto wao katika shule ambazo Kiingereza hutumika kama lugha ya kufundishia. Watu hawa husahau kuwa maarifa sahihi siku zote huja kwa lugha ya awali ambayo jamii husika wanatumia. Mataifa mengi duniani yaliyoendelea, lugha za kufundishia ni lugha za awali.

Katika kudhihrisha mapenzi yake kwa lugha ya Kiswahili, mwandishi hakuchelea kuipa sifa kuu ya Umama lugha hii. Katika shairi la ***Kiswahili Mama (uk. 39),*** mwandishi Amiri Sudi Andanenga anaiona lugha ya Kiswahili kuwa ni lugha tukufu katika kuandikwa na kusemwa kwake, hivyo anaiweka katika safu ya lugha zenye staha na heshima. Mwandishi anaifananisha lugha ya Kiswahili mithili ya ziwa la mama kwa namna ilivyo tamu kwa watumiaje wake. Hivyo, mwandishi anatuasa kuienzi na kuithamini kwani anaamini kuwa kupitia lugha hii adhimu jamii itaweza kujikomboa kiuchumi, kisiasa na kiutamduni. Katika ubeti wa tano wa shairi hilo, mshairi anasema:

**Hivyo lugha Kiswahili, ni la mama ziwa kama**
**Kama tukinyonya hili, na mengine tukakoma**
**Itasitawi miili, na kuponywa homahoma**
**Kiswahili ndie mama, nchini Tanzania.**

Leo tunaona baadhi ya Watanzania wanavyokosa umahiri na maarifa katika fani na stadi mbalimbali kwa vile tu lugha iliyotumika katika kupatia maarifa yao siyo lugha mama. Hivyo, Andanenga anaiasa jamii na kuinasihi Serikali ikubali kutumia lugha ya Kiswahili katika nyanja zote za maisha kwani ndiyo lugha mama na yenye tija kwa Watanzania. Na katika kudhihirisha mapenzi yake katika lugha hii kwa vitendo Andanenga amekuwa akishiriki vipindi na mijadala mbalimbali inayohusu lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, mtunzi ni miongoni mwa wanajopo wanaoongoza kipindi

cha Ulimwengu wa Kiswahili kinachorushwa na Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC). Aidha sauti yake imesikika katika mijadala, semina na makongamano ya lugha ya Kiswahili inayofanywa nchini.

Kwa kuhitimisha katika eneo hili, tumeona mwandishi ameweza kujadili dhamira mbalimbali, zilizojikita katika kuonya na kuelimisha jamii kuwa makini na mwenendo wa dunia. Dhamira nyingi zimeibua maudhi ya maonyo, mafundisho, maadabisho na uadilifu. Andanenga hakuwa mbali na maana ya maisha halisi, kwani dhamira zake zote hazitokani na ombwe bali zatokana na harakati na mazingira halisi ya jamii inayomzunguka. Kwa mantiki hiyo basi, dhamira zote zilizojadiliwa katika mjadala huu zimehalisika na mazingira halisi ya jamii. Lakini pia dhamira zimeumana sana na nadharia ya uhalisia ambayo ndiyo iliyotuongoza katika kubaini mchango wa kidhamira wa Andanenga katika ushairi wa Kiswahili.

### 4.3.1 Mchango wa Kimuundo wa Andanenga katika Ushairi wa Kiswahili

Mashairi ya Kiswahili yana miundo mingi. Baadhi ya vipengele vya muundo vinavyotumika zaidi ni mistari, beti, vina na mizani. Urefu wa mistari hutofautiana kutegemea mizani ya shairi husika au kutegemea mtiririko wa wazo au hisia. Urefu wa beti pia hutegemea idadi ya mistari. Hivyo katika hali kama hiyo zipo tungo zenye uwili *(mathna),* utatu *(Tathlihta),* unne *(Tarbiya),* utano *(Takhmisa),* usita *(Sudusia)* pamoja na mpangilio wa vina na mizani ikitegemea ubunifu na umahiri wa mshairi.

Andanenga ni mfuasi na muumini mzuri wa mashairi yanyozingatia arudhi za ushairi wa Kiswahili ambayo kwayo urari wa vina na mizani ndiyo uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili. Hili linathibitika kutokana na vitabu vyake vyote viwili vya

*Diwani ya Ustadh (1993)* na *Bahari ya Elimu ya Ushairi (2002)*. Mwandishi hajakiuka wala kukaidi kanuni za mashairi ya kimapokeo kama beti, mizani, vina, maana na utoshelevu. Mashairi ya kimapokeo yapo mengine yanajipambanua katika miundo na mitindo mbalimbali ya kifani katika kuusana ushairi wa Kiswahili.

Katika diwani zake zote mbili. Andanenga ameweza kutumia miundo na mitindo changamano ya ushairi wa Kiswahili kwa lengo la kuendeleza utanzu huu adhimu katika fasihi ya Kiswahili. Miundo kama *tarbiya, tathlitha, takhmisa***,** na mingi mingineyo imetumika katika diwani zake. Kadhalika baadhi ya miundo na mitindo mengine ni mipya na mingine ni ya kale inajitokeza katika utafiti huu. Baadhi ya mitindo na miundo aliyotumia ni kama vile: *mtiririko, ngonjera, msisitizo, tenzi, gungu, utumbuizi, ukawafi, wajiwaji, kidato, kisarambe, duril- mandhuma* na kadhalika. Wengine miundo ya ushairi huiita bahari.

Katika *Diwani ya ustadh*, mtunzi ametamba sana na muundo wa mashairi wenye mistari minne *(Tarbiya)* huku akidhihirisha ufundi wake kwa kutumia mitindo mbalimbali ya uwekaji idadi ya mizani katika muundo huo. *Tarbiya* ni muundo ambao ubeti mmoja wa ushairi unakuwa na mistari minne pamoja na kibwagizo. Katika kitabu hiki mashairi mengi ni ya muundo wa *tarbiya* kuanzia shairi la kwanza la ***Mvunja kwao (uk. 17-18)*** hadi shairi la mwisho la ***Molina Tupe Nguvuzo (100-101),*** yote haya yamezingatia muundo huo katika mitindo anuai. Tuone mfano wa muundo huo katika ubeti wa kwanza na saba wa shairi la ***Azimio la Arusha (uk. 19-20)*** mshairi anasema:

**Ni nani anae guna, mbele ya sisi kaumu**
**Nani anae nong'ona, twataka kumfahamu**
**Tunataka kumuona, mjinga? Ana elimu?**
**Safari tumeazimu, kwenda kwenye ujamaa.**

**Tamati rasilimali, zibakie mumuhumu.**
**Zisitoke kwenda mbali, kabaila kudhulumu**
**Tangu sasa ni muhali, tunapinga udhalimu**
**Safari tumeazimu, kwenda kwenye ujamaa.**

Beti hizo zina mishororo minne. Kila mshororo una vipande viwili vyenye mizani nane-nane (8/8) ambayo inakamilisha jumla ya mizani kumi na sita kwa mshororo mzima. Katika shairi hilo tunaona vina vya kati katika kila ubeti wa shairi hili vikitofautiana lakini vina vya mwisho vya shairi zima vikifanana ambavyo vinaishia na silabi ***-mu***.

Muundo huu pia ulitumiwa sana na mshairi maarufu wa Zanzibari Haji Gora Haji katika diwani yake ya *Kimbunga (1995),* kuanzia shairi la ***kimbunga (uk.1-2)*** hadi shairi lake la ***Deni (uk.32)*** anaonekana kutumia sana muundo wa *tarbiya* katka mwendo wa mizani ya 8/8.

Kadhalika katika *Bahari ya Elimu ya Ushairi* mtunzi pia ametumia muundo wa mashairi ya *tarbiya* yenye mizani nane (8/8) kwa kila kipande katika mshororo mmoja wa kila ubeti ukikamilisha mizani kumi na sita. Katika shairi la ***Umbo lake ni pambo (uk. 93), Jiunge na kila jema (uk. 90),*** mwandishi ameweza kutamba na muundo wa tarbiya kwa kiasi kikubwa. Tuone mfano wa ubeti wa kwanza katika shairi la ***Umbo lake ni pambo,*** na hapo anasema:

**Hakika ya wangu wimbo, habibu umeridhia**
**Ya kwamba mke ni pambo, kama nilivyokwambia**
**Limekwisha lote jambo, ambalo ukibishia**
**Mke pambo la Dunia, kazi yake kutupamba.**

Lakini katika shairi la ***Pongezi (uk. 90-91)*** mtunzi ameweza kuonesha ustadi wake huku akitunga *tarbiya* yenye mizani kumi na nane ikiwa na vipande vitatu katika mshororo mmoja na kila kipande kikiwa na mizani sita yenye vina (18: 6/6/6). Huu ni mtindo adimu kidogo katika uga wa mashairi ya kimapokeo. Tuone mfano wa muundo huo katika ubeti wa kwanza wa shairi hili;

**Tungo za aina, ya ubeti wako, juu nilopanga**
**Endelea sana, mashikoni mwako, daima kutunga**
**Ikiwezekana, mwambie mwenzako, yule chapapunga**
**Awache kunena, yenye matapiko, tungo kuboronga.**

Mwandishi akidhihirisha ubingwa wake wa kutamba na miundo na mitindo kadha wa kadha ya ushairi wa Kiswahili ameweza pia kutunga mashairi ya muundo wa *tarbiya* wenye mizani kumi na mbili katika kila mshororo wa ubeti ambao ni wa mizani sita katika kila kipande cha mshororo, kwa kuwa na mwendo wa shairi la: 6/6, *tarbiya*. Huu ni mtindo wa vipande vifupi. Katika *Diwani ya Ustadh* muundo huu unaonekana katika shairi la ***Fanya ulizio (uk.88).*** Ubeti wa kwanza, anaandika hivi:

**Leo nina jambo, nataka kwambia**
**Sikiza mrembo, badili tabia**
**Mapenzi ya shombo, sitavumilia**
**Nataka mapambo, sitaki udhia.**

Katika diwani ya *Bahari ya Elimu ya Ushairi* mtunzi ametufunza kuandika mashairi yenye muundo wa mizani kumi na mbili katika mgawanyiko wa mizani 4/8 na 8/4, *tarbiya*. Miundo hii tofauti nayo ni nadra kuonekana katika kambi ya ushairi wa

kimapokeo. Katika shairi la ***Ahadi (uk.74- 75)*** katika ubeti wa tatu na katika shairi la ***Tuzindushane (uk.76)*** ubeti wa pili, mshairi atongoa:

**Jambo jema, ahadi ukiahidi**
**Ni lazima, kuitimiza ahadi**
**Ukisema, kamwe nyuma usirudi**
**Toa dhima, impendeze wadudi.**

**Nawe pia usitake, ukitaka**
**Uwe mume uwe mke, si dhihaka**
**Kamwe usidanganyike, sala shika**
**Kesho tukakubalike, na Rabuka.**

Beti mbili za hapo juu zinatuonesha uwezo wa mshairi kutunga na kutumia muundo wa shairi lenye mizani 12 katika mwendo wa shairi 4/8 na 8/4, *tarbiya*. Kwa mujibu wa Andanenga, anadai kuwa miundo hii ya mizani kumi na mbili katika mwendo wa 4/8 na 8/4 mara nyingi hupatikana katika mtindo wa *wimbo.*

Zaidi ya hilo, mtunzi ametumia muundo wa *tarbiya* huku akijitokeza katika mtindo wa *Utumbuizi*. Huu ni mtindo wa shairi lenye mizani kumi na nne katika kila mshororo. Mshororo una vipande viwili katika mwendo wa 8/6 au 6/8. Kwa mujibu wa mwandishi anadai kuwa: *"mshororo huo pia unaweza kugawanyika katika vipande vitatu, 6/4/4 au 5/4/5 na vipande vyote huwa na kina".* Katika *Bahari ya Elimu ya Ushairi* muundo huu umeoneshwa katika shairi la ***Hatubandukani (uk.83)*** ambao ubeti wa kwanza unajieleza hivi:

**Ni kama ruba, kwenye moyo, ameniganda**
**Ni kwa mahaba, yake huyo, kwa kunipenda**
**Amenishiba, zenu payo, hazitashinda**
**Ni kabakaba, anipayo, pendo la wanda.**

Katika ubeti huo juu, mwandishi anaonesha umahiri wake wa kuweza kutunga muundo wa *tarbiya* katika mtindo wa *utumbuizi* yaani shairi lenye mizani kumi na

nne akituonesha uwezo wa kutumia utunzi wa vipande vitatu kila mstari katika mwendo wa shairi: 5/4/5.

Kadhalika katika kuonyesha ubingwa wa kusarifu na miundo mbalimbali ya ushairi wa Kiswahili mtunzi pia ameweza kutunga mashairi ya *tarbiya* yaliyo katika mtindo wa *Kidato* kwa lengo la kuundeleza ushairi wa Kiswahili kimuundo. Andanega (2002:122) anaeleza kuwa *kidato* ni mtindo wa shairi linaliotungwa kwa mwendo wa mishororo minne au zaidi kwa mpango wa mizani 8 kwa 8 kama mwendo wa shairi.

Mtunzi anatujuvya kuwa mwendo wa kidato una masharti yake katika kutunga kwake: maneno yanayoanzia katika mshororo wa kwanza, watatu na wa nne au zaidi hurudiwa katika beti zote, mizani nane katika kipande cha mwisho cha mshororo wa nne au zaidi hurudiwa katika beti zote. Kila ubeti huwa na vina vyake, kina cha mwisho cha ubeti wa kwanza huwa kina cha kati *(kina awali)* na katika ubeti wa pili na kuunda kipya katika ubeti wa pili mwisho *(kina tamati).* Ambacho kitakuwa kina cha kati katika ubeti wa tatu, na kuunda kina kipya cha mwisho katika ubeti wa tatu mwishoni. Mwendo huu huendelea hadi mwisho wa shairi. Ni mtindo ambao unaweza kutunga shairi refu bila kumchosha msomaji. Aidha ni mtindo ambao mtunzi anaweza kutoa mawazo yake kwa undani sana. Katika kitabu cha *Bahari ya Elimu ya Ushairi* mtunzi ametufunza na kutuonesha namna ya utunzi wa muundo huu akitumia shairi la ***Iandae kesho yako (uk.122-123)*** na ***Watengeza kwa wenzao (uk.124-125).***

Hebu tuone mfano wa muundo huu katika shairi la ***Watengeza kwa wenzao*** ubeti wa tano na wa sita katika mwendo wa shairi: 8/8, tarbiya:

***HABIBU*** **wajibabua, kofi shavuni mwenyewe**
**Pia kwenye yako pua, waibamiza kwa mawe**
***BILA*** **hata kupumua, wajisifu kwa mayowe**
***KWA*** **kujisibu mwenyewe,** ***SIWEZI KUKULILIA.***

***HABIBU*** **mwenzangu wewe, wajivunjia heshima**
**Unaridhi uzomewe, kwako kunademadema**
***BILA*** **shaka ni kiwewe, mno kimekusakama**
***KWA*** **vile unajichoma,** ***SIWEZI KUKULILIA.***

Muundo huu wa shairi ulishawahi pia kutumiwa na washairi wengi akiwemo gwiji wa ushairi wa Kiswahili Hayati Mathiasi Mnyampala katika muswada wa *Mashairi ya Vidato (ht)* akitumia shairi la ***Kitung'ati (uk.6).***

Katika *Bahari ya Elimu ya Ushairi* mtunzi anatuonesha muundo wa mashairi ya *tarbiya* katika mtindo mwengine uitwao *Zingo.* Zingo ni aina ya shairi linalotungwa kwa kutumia neno la mwisho katika mshororo wa kwanza, huku mwishoni huwa mwanzo katika mshororo wa pili, na neno la mwisho katika mshororo wa pili huanzia katika mshororo wa tatu, na lile la mwisho katika mshororo wa tatu huanzia katika mshororo wa nne na kuendelea( Andanenga, 2002: 133-138).

Neno la mwisho katika mshororo wa mkarara, limetumika hilohilo katika kila ubeti unaofuata. Neno la mwisho katika ubeti limetumika kuanzia mstari wa mkarara. Na la mwanzo la mkarara na la mwisho yanajirejea. Mtindo huo huitwa "*Pete kuu"* ambayo huunganisha beti zote za shairi. Tuone mfano ufuatao wa *zingo* katika shairi la ***Nasaha (uk.133-134)*** una mwendo wa shairi: 8/8, *tarbiya.*

**Zipokeeni salamu, marafiki wa *Mvita***
***Mvita* wa taalamu, kwa kupata njema *nyota***
***Nyota* bora ni vigumu, watu wabaya *kupata***
***Kupata* wenye kufata, kwa kuyatenda *mazuri.***

***Zuri* katika Dunia, tuombe *yanayoleta***
***Yanayoleta* hisia, nzuri si ya *matata***
***Matata* kuyafukia, ili pepo *kuipata***
***Kuipata* kwa kupita, katika mambo *mazuri.***

Katika beti mbili hapo juu ambazo wengine huita *Pete kuu* ni neno *mazuri* kama yalivyo maneno yote yanayopatikana mwishoni katika kipande cha pili cha ubeti ndicho kinachoanza katika kipande cha kwanza katika mshororo unaofuata. Hii inaonesha umahiri na uwezo mkubwa wa kifani hasa katika usanaji wa kimuundo alionao mwandishi.

Kadhalika katika muundo huu mtunzi pia ametufunza na kutuonesha mtindo wa *Zingo la mkufu.* Zingo la mkufu ni shairi linalotungwa kwa kukata silabi za neno la kati, na kipande chake cha silabi mbili la neno hutumika kuanzia mshororo huohuo. Neno la mwisho la mshororo huo hukatwa silabi mbili ambazo ni sehemu ya neno mwanzoni mwa mshororo wa pili (Andanenga, 2002:134). Mshairi akitumia mashairi ya ***Nasaha (uk.133- 134), Winda (uk. 136-137), Nakuja (uk.137), Mjuzi majambo (uk. 136-137)*** na ***Kweli (uk. 138)*** mtunzi anaudhihirisha muundo huu kwa weledi mkubwa. Hebu tuone mfano mmoja ya hiyo katika shairi la ***Mjuzi majambo*** katika ubeti wa kwanza na wa pili ukiwa katika muundo wa shairi la mizani 8/8, anasema:

**Ndimi mjuzi ma*jambo*, JAMBO likikaka*wana***
**WANA hupigwa vi*kumbo*, KUMBO watu hutu*pana***
**PANA nguvu za mi*tambo*, TAMBO kwa kutambi*ana***
**ANA kwa kuweze*kana*, KANA kwamba ni ja*siri.***

**SIRI yataka he*kima*, KIMA cha malele*mwana***
**MWANA anaposi*mama*, MAMA na Baba hu*ona***
**ONA wanavyoji*pima*, PIMA jibu huki*nena***
**NENA jambo la ku*fana*, FANA utakavyo*weza*.**

Muundo na mtindo huu wa ushairi wa *zingo* na *zingo la mkufu* umewahi kutumiwa pia na baadhi ya washairi kama vile Ustadh Abdullatif Abdala wa Mombasa kama alivyonukuliwa na Andanenga (2002:134-137) katika shairi la ***Tulia (uk.134)*** na ***Nnakuja (uk.137).*** Naye Muhammed Seif Khatib ndani ya diwani ya *Wasakatonge (2005)* katika uga wa washairi wa zama hizi amewahi kutumia muundo na mtindo huu katika shairi lake la ***Nahodha (uk.41-42).***

Katika kuonesha uwezo wake wa kutunga mashairi katika miundo na mitindo mbalimbali kwa lengo la kuendeleza ushairi wa Kiswahili, Andanenga anaonesha kwa kutumia mashairi ya mtindo wa *Dhivendo* yakiwa katika muundo wa *tarbiya* katika mwendo wa shairi: 8/8.

Andanenga ( 2002:146) anaeleza kuwa, *dhivendo* ni aina ya mtindo wa utungaji ambao katika mishororo yake yote huanza na neno hilohilo, yaani kwa msemo wa kishairi ni *" takriri neno awali".* Mtindo huu wa mashairi ulishawahi pia kutumiwa na magwiji wengi wa ushairi wa Kiswahili, baadhi yao ni kama vile Mathiasi Mnyampala katika *Diwani ya Mnyampala (1965)* akitumia mashairi ya ***Wastara Hazumbuki (uk.8)*** na ***Urafiki Tufanane (uk.8-9)*** na Akilimali Snowhite katika *Diwani ya Akilimali (1966)* akitumia shairi la ***Ua la Moyoni (uk.14).*** Katika kitabu

cha *Bahari ya Elimu ya Ushairi* muundo huu unapatikana katika shairi la ***Sema (uk. 146- 147).*** Tuone mfano huo katika ubeti wa tatu na nne kama hivi:

***Sema* yanayotakiwa, yasiyo mbaya athari**
***Sema* kama waelewa, ya kweli si ya ghururi**
***Sema* mema kwa kupewa, mema na mola kahari**
***Sema* maneno mazuri, kila baya usiseme.**

***Sema* yalo na hakika, nisemayo sikughuri**
***Sema* mambo muafaka, kwa watu yakidhihiri**
***Sema* usijepotoka, kesho ukapata nari**
***Sema* maneno mazuri, neno bovu usiseme.**

Na katika *Diwani ya Ustadh,* muundo huu wa ushairi umetumika katika mashairi ya ***Jinga (uk. 66),*** na ***Pendo la pesa (uk. 91).*** Tuone mfano katika shairi la ***Jinga*** ubeti wa tatu unasema:

***Jinga* lanuka uvundo, harufu mbi hutoka**
***Jinga* liwekeni kando, msije mkatapika**
***Jinga* linao mfundo, moyoni limeuweka**
***Jinga* limekwerevuka, halino si jinga tena.**

Katika mifano ya beti hizo hapo juu itabainika kuwa neno *sema* katika shairi la Sema lipo mwanzo wa kila mshororo na kuwepo pia katika kila ubeti wa shairi mpaka mwisho. Neno *jinga* kadhalika, linapatikana mwanzoni mwa kila kipande cha kwanza katika mshororo na kila ubeti wa shairi kuanzia mwanzo hadi mwisho wa shairi.

Akitamba na kuambaa zaidi katika muundo huu, Andanenga ametumia na kutubainishia mtindo wa *Dhivendo pata*. Kwa maelezo yake mtunzi anafafanua kuwa: *"Dhivendo pata ni aina ya shairi linalotungwa kwa kurudia neno lilelile mwanzo na kati katika mshororo. Neno ambalo hurejewa na hukaririwa tena katika*

*kila kipande cha mstari".* Muundo huu wa shairi umetumika katika shairi la ***Umbea (uk. 74).*** Ubeti wa saba wa shairi wa katika *Diwani ya Ustadh,* unasema:

***Umbea* mbaya adabu*, umbea* si matukuza**
***Umbea* mbaya kulabu*, umbea* katu kukuza**
***Umbea* si unaibu*, umbea* hukandamiza**
**Si kitu cha kupendeza, umbea unaharibu.**

Na katika kitabu cha *Bahari ya Elimu ya Ushairi, dhivendo pata* inapatikana katika shairi la ***Piga (uk.147- 148)***. Mfano upo katika ubeti ufuatao:

***Piga* ngoma isikike*, piga* ili tuicheze**
***Piga* sana usichoke*, piga* usijilegeze**
***Piga* kwa mdundo wake*, piga* nyoyo tusuuze**
***Piga* ngoma ipendeze*, piga* anga izagaze.**

Katika beti nilizozinukuu hapo juu, utabaini kuwa neno *umbea* na neno *piga* yanajitokeza mwanzoni katika kila kipande cha mshororo yaani kipande cha kwanza na mwanzo wa kipande cha pili cha mshororo. Utaratibu huo huenda hivyohivyo kuanzia ubeti wa kwanza wa shairi mpaka wa mwisho.

Katika kudhihirisha umahiri wake wa kucheza na miundo na maneno katika ushairi wa Kiswahili, Andanenga katika *Bahari ya Elimu ya Ushairi* sasa anatuonesha tungo ya *Gungu*. Hili ni shairi lenye mizani kumi katika kila mstari kwa mpangilio wa mizani 4 na 6, katika *tarbiya*. Aghalabu *gungu* huwa na mistari minne, na silabi ya mwisho ya kila mstari ni kina cha shairi zima. *Gungu* mara nyingi kiasili huko Lamu na Pate ni shairi linaloimbwa. Katika shairi la ***Wamezama (uk.41)*** mtunzi anatuonesha namna gungu inavyotungwa. Katika ubeti wa nne wa shairi twaoneshwa mfano wake:

**Zote nyundo, zisizo huruma**
**Nazo tindo, zikitinda vyuma**
**Pia nondo, zisizopindama**
**Viko kando, chini vimezama.**

Katika ubeti hapo juu twaona kuwa kipande cha kwanza cha kila mshororo kina mizani minne, na kipande cha pili kina mizani sita, hivyo kukamilisha idadi ya mizani kumi. Na silabi ***-ma*** katika kila kipande cha mwisho cha mstari ndiyo kina cha shairi zima.

Fauka ya hilo, mtunzi pia ametumia muundo wa mashairi yenye mizani kumi na moja katika mtindo wa *Kisarambe*. Mtindo wa kisarambe umetungwa na watunzi wengi wa sifa katika dahari zao. Mshairi na maarufu wa ushairi wa Kiswahili Kaluta Amri Abeid (1954) alitumia mtindo huu katika shairi lake la ***Wimbo wa Nai (uk.25).*** Lakini pia mshairi maarufu wa Mombasa Ahmad Nassir Juma (1970) ametunga shairi refu katika mwendo wa *Kisarambe* linaloitwa ***Mwanaadamu (uk.116).*** Tunukuu beti ifuatayo ya mwandishi huyo na tuone inavyoonekana.

**Ukitaka amba, la mtu sambe**
**Na mtu kuomba, usimuombe**
**Muombe muumba, mpa viumbe**
**Asipo kupamba, usijipambe.**

Katika Kisarambe tunaona neno la mwisho la kipande cha kwanza cha mstari kinapata neno la kinyume mwisho wa mstari wa kipande cha pili. Lakini siyo lazima iwe hivyo. Muundo huu huwa na mizani sita katika kipande cha kwanza cha mshororo na mizani mitano katika kipande cha pili cha mshororo na kuwa na mwendo wa mizani kumi na moja 6/5, katika *tarbiya.*

Katika *Diwani ya Ustadh,* muundo huu umejitokeza katika shairi la ***Sauti ya kiza (uk.93)*** katika ubeti wa tisa wa shairi lakini haufati neno la kinyume chake kama ilivyokuwa hapo juu. Mshairi anaandika:

**Tamati nafunga, Kwa kuishia**
**Mato ndo malenga, kanikimbia**
**Nahofu kutunga, mabeti mia**
**Asije chukia, ayasomaye.**

Mshairi Andanenga ametumia muundo wa *tahtlitha (utatu)* katika mashairi yake. *Tahtlitha* ni shairi lenye beti za mishororo mitatu. Linaweza kuwa katika mizani kumi na sita yenye vipande viwili vya nane kwa nane (8/8) au vyengine katika kila mshororo. Katika *Bahari ya Elimu ya ushairi* mtunzi ametumia muundo wa *tathlitha* katika shairi la ***Zizamile kupi (uk. 87- 88)*** lenye mizani kumi na sita katika kila mshororo wenye vipande viwili vya mizani nane kwa nane. Ubeti mmoja wa tathlitha ni kama ufuatao;

**Ikupi ile elimu, ikisomeshwa zuoni**
**Niko radhi kugharimu, na iwe kwa bei gani**
**Naambiwa ni vigumu, asaa chuma laini.**

Muundo huu pia wa tathlita yenye mizani kumi na sita katika mwendo wa 8/8 uliwahi kutumiwa na washairi maarufu katika uga huu kama vile Nassir, A katika kitabu chake cha *Malenga wa Mvita (1970)* akitumia shairi la ***Wosia (uk.109)*** na Kaluta Amri Abeid (1954) akitumia shairi lake la ***Manani (uk.75).***

Katika shairi la ***Siendekeze moyo (uk. 88- 89)*** mtunzi pia ametumia *tathlitha* yenye mistari mitatu ya mizani nane yenye kina -***si*** kwa kila mstari wa beti zote za shairi hilo. Muundo huo katika ubeti wa tatu wa ashairi unasema:

**Wasia wangu halisi**
**Kwangu na kwa wangu mbasi**
**Kumcha wetu Qudusi.**

Katika *Diwani ya Ustadh,* mtunzi pia ametumia muundo wa mashairi ya mistari mitatu *(tathlitha).* Ingawa muundo huu haukutamalaki sana katika kazi za mshairi huyu. Katika shairi la ***Ni (uk. 50)*** mwandishi anadhihirisha uhodari wake kwa kutunga mashairi ya *tahtlitha.* Katika shairi hili ameleta kibwagizo chenye mizani nane na mwisho kuuliza swali. Ni muundo adimu! Anatongoa hivi:

**Andanenga nikisema, naambiwa hayawani**
**Eti bado naloloma, kama debe upeponi**
**Ninavunjiwa heshima, na kufanywa thama duni**
**Sasa mumeniamini?**

Muundo huu wa kuuliza swali mwisho unaweza kuwa adimu wa ubunifu wake, umeigwa na kuwaathiri pia washairi wa diwani ya *Malenga Wapya (1997)*, katika shairi lao la ***Kwanini? (uk.1-2).***

Muundo wa *tathlitha* huweza pia kugawanywa katika vipande vitatu vya 6/4/4 au 5/4/5 na vipande vyote huwa na kina. *Tathlitha* ikiwa katika umbo la vipande vitatu huitwa *Utumbuizi*. Katika kitabu cha *Bahari ya Elimu ya Ushairi* mtunzi ameutumia muundo huo katika shairi la ***Heshima kwa Wazazi (uk.84)***. Mfano wa *tathlitha* katika mwendo wa 5/4/5 unajitokeza hivi katika ubeti wa tatu wa shairi;

**Nini tulipe, yalingane, yao matendo**
**Mema tuwape, si kingine, chenye muundo**
**Yangu meupe, tushikane, kwenye upendo.**

Naye mshairi mahiri na maarufu wa zama hizi katika uga wa ushairi wa Kiswahili Muhammed Seif Khatib, katka Diwani yake ya *Wasakatonge (2003)* anaonekana

kuathiriwa na muundo huu wa *tathlitha* wenye vipande vitatu kwa mshororo mmoja katika shairi la ***Tohara (uk.2-3)***. Yeye akaongeza na kibwagizo cha mizani mitatu chenye kusisitiza maudhui yake. Lakini pia ametunga tathltha yenye mizani kumi na sita kwa mwendo wa 8/8 katika shairila ***Itoe Kauli Yako (uk.27)*** na tathlitha yenye mizani kumi na mbili kwa mwendo wa 6/6 ndani ya shairi la ***Usiku wa Kiza (uk.27-28).***

Andanenga ameweza kutumia muundo wa mashairi yenye mistari mitano *(Takhmisa)*. Inaaminika kuwa mwasisi wa muundo huu ni gwiji wa ushairi wa zama hizo Sayyid Abdallah Bin Ally Bin Nassir (1720-1820). Yeye ni mtunzi wa tungo tatu, *Utenzi wa Al-Inkishafi*, Takhmisa ya Lyongo na Wajiwaji (Mulokozi, 1999). Naye, gwiji wa fasihi na ushairi wa Kiswahili Shaaban Bin Robert aliwahi kutumia muundo wa takhmisa katika mashairi yake. Kwa hiyo katika Diwani ya *Kielelezo cha Fasili (1973)* alitumia muundo huu katika shairi la ***Ajabu tupu (uk. 27)***. *Takhmisa* ni muundo wa shairi lenye mishororo mitano katika kila ubeti. Katika *Diwani ya Ustadh*, Andanenga ametumia muundo wa *takhmisa* katika shairi la ***Mdodoso (uk. 52).*** Katika shairi hilo mtunzi amelisana shairi lake kwa ustadi mkubwa huku akitumia muundo wa takhmisa wenye mwendo wa shairi la mizani 8/8 kwa kila kipande na huku likikamilisha idadi ya mizani kumi na sita katika kila mshororo. Katika ubeti wa kwanza wa shairi hilo mwandishi anatongoa;

**Utyata hili shairi, mtungo wa takhmisa**
**Mtunzi ndimi Amiri, mtafutaji makosa**
**Na leo yangu dhamiri, ndugu yangu kudodosa**
**Ili tutafute heri, tuiembete kwa hasa**
**Na ikiwa ipo shari, ni haki kuipukusa.**

Katika *Bahari ya Elimu ya Ushairi*, mtunzi ametumia muundo wa mashairi ya *takhmisa* kwa lengo la kuendeleza utanzu huu kifani hasa katika kipengele cha

muundo. Akitumia shairi la ***Wasia (uk. 97- 98),*** Andanenga anadhihirisha uwezo wake wa kutunga *takhmisa* yenye muundo wa mizani ya 8/8 na kwa jumla ya yote ni mizani kumi na sita kwa kila mshororo lakini kila mshororo ukiwa unatofautiana na mwingine kwa vina na kila mshororo ukiwa na vina vinavyofanana vya kati na mwisho. Ubeti wa tano wa shairi hilo linadondoa hivi:

**Mtu mwema ni ada*bu*, kuwa nayo ni waji*bu***
**Waone watu ni wa*tu*, ili nawe uwe m*tu***
**Aidha yawalaz*imu*, wenzenu kuwaheshi*mu***
**Wazazi baba na ma*ma*, kuwaheshima laz*ima***
**Aidha na majira*ni*, wapewe kila hisa*ni*.**

Andanenga pia ameonesha uwezo wa kutunga mashairi yenye muundo ya *uwili (Mathna),* yaani beti zina mishororo miwili zikijitokeza katika mitindo mbalimbali ya ushairi wa Kiswaili. Katika *Bahari ya Elimu ya Ushairi* mtunzi anautumia muundo huu kupitia shairi la ***Jiepushe (uk. 85-86)*** lenye mwendo wa shairi: 8/8 likikamilsha idadi ya mizani kumi na sita kwa kila mshroro. Katika ubeti wa nne wa shairi hilo linasomeka hivi:

**Jiepusha na fitina, kwa mbali na majirani**
**Ufitina ni laana, machukizo kwa manani.**

Kadhalika mtunzi ameweza pia kuonesha uwezo wake wa kutumia muundo wa *mathna* katika mtindo wa mizani kumi na mbili katika mwendo wa 6/6. Akitumia shairi la ***Jana na leo (uk. 86)*** katika ubeti wa kwanza na wa pili, anasema:

**Jana ishapita, uwe waitaka**
**Kwa kuifuata, hautaishika.**

**Leo imefika, usikawilie**
**Ipe zako twika, ikutumike.**

Aidha Andanenga amefanikiwa kudhihirisha uwezo wake wa kucheza na muundo wa mashairi ya *uwili* akitumia mtindo wa mizani nane katika mshororo na kila kipande kikiwa na mizani ya nne: 4/4. Katika *Bahari ya Elimu ya Ushairi* akitumia shairi la ***Wako wapi? (Uk. 173-174).*** Amebainisha umahiri huo katika ubeti wa kwanza na wa pili, anasema:

**Wako wapi, wa mishipi**
**Kwa kifupi, nauliza.**

**Kwenye vyombo, wenye mambo**
**Bila chambo, wakivuza.**

Katika beti hizo tunaona kuwa kipande cha kwanza na kipande cha pili cha mstari wa kwanza na kipande cha kwanza cha mstari wa pili vina vinavyofanana vya ***-pi***. Tunaona ubeti wa pili katika kipande cha kwanza mstari wa kwanza na mstari wa pili kina cha kati kinafanana ambacho ni ***-mbo***. Hata hivyo kina cha mwisho katika beti zote ni ***-za.***

Kwa upande mwingine mtunzi ametumia muundo adimu wa ushairi wa *Sudusia (Usita)*. Huu ni muundo ambao mashairi hutungwa kwa idadi ya mishororo sita katika kukuamilisha ubeti wa shairi. Katika kuonesha uwezo wake wa kuunda miundo mbalimbali ya ushairi wa Kiswahili, Andanenga ameutumia muundo huu katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili. Katika kitabu cha *Bahari ya Elimu ya Ushairi,* mtunzi ametumia muundo *Sudusia* katika shairi la ***Mlango wa Kheri (uk. 98-99)*** huku akisisitiza washairi wengine kujitoma katika matumizi ya muundo huo kwa lengo la kuimarisha sanaa ya ushairi wa Kiswahili. Ubeti wa tano wa shairi anadondoa:

**Kaditamati shairi, la mwendo wa sudusia**
**Na nyinyi nawashauri, mwendo huu kutungia**
**Ushairi ni bahari, lulu twende jivulia**

**Mimi mwenzenu tayari, nimekwisha tumbukia**
**Wenzangu msitakhari, njooni nawagutia**
**Bali tutende kwa ari, humu nilohadithia.**

Muundo huu pia ulishawahi kutumiwa na nguli wa ushairi wa Kiswashili hayati Shaaban Robert ndani ya kitabu chake cha *Pambo la Lugha (1966),* akitumia shairi la ***Viumbe Twachosha (uk.74).***

Andanenga katika mawanda mengine amejaaliwa wasaa wa kutunga mashairi akitumia muundo na mtindo wa mashairi ya *Mtiririko.* Mtiririko ni shairi linalotungwa kutumia vina viwili katika shairi lote. Mathalani kama vina vya mwanzo vya shairi ni ***-ma*** na vya mwisho ni ***-ka*** basi shairi zima huenda katika mapigo hayo ya kisilabi kuanzia ubeti wa kwanza hadi wa mwisho. *Mtiririko* huu aghalabu hupatikana katika muundo wa *tarbiya* wenye mwendo wa shairi: 8/8 likiwa na mizani kumi na sita. Inasadikiwa muundo na mtindo huu wa ushairi uliasisiwa na mshairi maarufu wa ushairi wa Kiswahili Mathiasi Mnyampala akitumia shairi lake la ***Tungeni mtiririko (uk.5-6)*** katika *Diwani ya Mnyampala (1965).* Washairi wengi wanautumia muundo huo hivi sasa.

Andanenga naye amefanikwa kutumia muundo huu kwa kiasi kikubwa katika utunzi wake wa mashairi mengi ambayo yamo katika vitabu vyake. Katika *Diwani ya Ustadh* muundo huu umetumika katika mashairi ya ***Tuiunde nchi yetu (uk.32), Dhamira ya nchi yetu (uk. 34), Kitangazwe Kiswahili (uk. 38), Kiswahili kipambwe (uk.44), Piga kama Mpigaji (uk. 65), Kutowa (uk.80), Ya Allahu ya Robati (uk.95)*** na shairi la ***Moyo na macho (uk. 81).*** Katika kitabu cha *Bahari ya Elimu ya Ushairi*

mtindo huu umetumika katika mashairi ya ***Semeni (uk.139)*** na shairi la ***Wazazi (uk.140-141)***. Tulione moja ya mashairi hayo katika shairi la ***Ya Allahu ya Robati (uk. 95).*** Ubeti wa kwanza, pili na wa tatu anabainisha hivi:

**Makelele na vibwa*to*, vilisikika waka*ti***
**Tulipopata mite*to*, kuwa Shabani mau*ti***
**Nyoyo zikawa nzi*to*, kutoka ngome thabi*ti***
**Likampate Robati, fukisho la manukato.**

**Fukisho la manuka*to*, likampate Roba*ti***
**Na wazee wa mto*to*, msizidishe buhu*ti***
**Kwani huo ndio mwi*to*, wote kwetu utafi*ti***
**Likampate Robati, fukisho la manukato.**

**Shabani wake mvu*to*, kauacha kwa uma*ti***
**Mvuto wake Amba*to*, utunzi wa zake ha*ti***
**Nyingi kama virobo*to*, kwetu zimekuwa vi*ti***
**Likampate robati, fukizo la manukato.**

Katika beti hizo tatu hapo juu utagundua kuwa kuna mtiririko wa vina vinavyofanana vya mwanzo na mwisho. Katika vipande vya kwanza vya kila ubeti vina vyote vimeishia na silabi ***-to*** na katika vipande vya pili vya kila ubeti vina vyote vimeishia na silabi ***-ti*** kuanzia ubeti wa kwanza wa shairi hadi ubeti wa mwisho wa shairi.

Kadhalika katika *Bahari ya Elimu ya Ushairi* mtunzi ameweza kutumia muundo wa *mtiririko* katika shairi la ***Semeni (uk.139-140)*** na shairi la ***Wazazi (uk. 140-141).*** Katika shairi la Semeni mwandishi anatumia vina vya ***-ii*** katika vipande vya mwanzo vya kila ubeti na ***-ma*** katika vipande vya mwisho vya kila ubeti vikiwa katika mwendo wa shairi: 8/8 muundo wa *tarbiya* kuanzia ubeti wa kwanza hadi wa mwisho wa shairi. Katika ubeti wa kwanza wa shairi hilo mshairi anatongoa:

**Na ingawa niko j*ii*, msidhani nimeha*ma***
**Mkadhani sisik*ii*, hivyo mnavyolala*ma***
**Tabia yangu ut*ii*, kuwa nayo sitako*ma***
**Semeni mtayosema, mimi siwazuilii.**

Na katika shairi la *Wazazi* kina cha ***-li*** katika kipande cha kwanza cha kila mshororo na kina cha ***-ma*** katika kipande cha pili cha kila mshororo vinajitokeza katika beti zote ukiwa katika mwendo wa shairi: 8/8, *tarbiya.* Katika ubeti wa tatu wa shairi, msanii anaimba:

**Tulipokuwa tunga*li*, watoto wazazi a*ma***
**Wazazi kwa maadi*li*, walikuwa kwenye hi*ma***
**Wenyewe walijidhi*li*, kwa tiba katika ho*ma***
**Tupende Baba na Mama, wazazi wetu wawili.**

Kadhalika mwandishi ameweza kutamba na muundo wa mashairi ya *Msisitizo*. Huu ni muundo wa ushairi ambao hutungwa kwa mpango wa mishororo sita *(Sudusia)* au mishororo mitano *(Takhmisa)* ambayo aghalabu hubeba mizani 16 kwa mkao wa mizani 8/8, isipokuwa mshororo wa tatu ambao huwa na mizani 8 tu. Mshororo ambao neno lake la mwisho husisitiza katika neno la kwanza la katika mshororo wa nne. Inasadikiwa muundo huu wa ushairi uliasisiwa na shaha wa ushairi wa Kiswahili hayati Mathiasi Mnyampala katika Diwani ya *Waadhi wa Ushairi (1965)* akitumia shairi kama ***Nikaze yangu nira (uk. 122)*** na ***Natunga msisitizo (uk.120)*** na baadaye akamuathiri nguli wa fasihi na ushairi wa Kiswahili hayati Shaban Robert alipotunga shairi la ***Kiunzi chetu (uk.18)*** ndani ya diwani ya *Sanaa ya Ushairi (1970).*

Andanenga ametumia muundo huu kwa makusudi ya kuendeleza ushairi wa Kiswahili hasa akijikita katika kuisana kazi yake kimuundo. Katika *Diwani ya Ustadh* muundo huu umetumika katika mashairi ya ***Ujengaji wa Taifa (uk.22), Msitu (uk. 67)*** na ***Zamani haiji (uk. 99)*** na katika *Bahari ya Elimu ya Ushairi* muundo huu umetumika katika mashairi ya ***Risala (uk.127-128), Pambo la mke (uk. 128-130), Kitendawili (uk.130-131)*** na ***Nyanyaso la jinsia (uk. 131- 132).*** Katika

shairi la ***Msitu (uk.67)*** ubeti wa kwanza na shairi la ***Zamani haiji (uk.99)*** ubeti wa kwanza mshairi anaghani hivi:

**Msitu huu mnene, nausifia Amiri**
**Umejaza pande nne, kwa miti yake mizuri**
**Mizuri *imenawiri***
***Imenawiri* ione, imejaza mema furi**
**Twende tushirikiane, tuone yalo shimiri**
**Msitu una athari, twende kwa uangalifu.**

**Nilipokuwa mzima, maozi na zake mboni**
***Nisikieni jamni!***
**Kwa kuweza kutazama, kilicho juu na chini**
***Mbele nyuma na pembeni!***
**Niliweza kuvipima, kwa daraja na thamani**
***Leo haiwezekani!***

Katika beti hizo mtunzi ametumia muundo wa msisitizo wenye idadi ya mishororo sita *(Sudusia)* katika kuisana na kuinogesha kazi yake. Tofauti kubwa ya kimuundo iliyojitokeza katika beti hizo ni vipande vya *msisitizo*. Katika shairi la ***Msitu (uk.67)*** kipande cha msisitizo ni kimoja na kinapatikana katika mshororo wa tatu katika kila ubeti, wakati katika shairi la ***Zamani haiji (uk.99)*** vipande vya msisitizo ni vitatu na vinapatikana katika mshororo wa pili, nne na sita katika kila ubeti. Andanenga anaonekena kuusana vizuri mtindo huo ambapo mwasisi wa muundo huo hakutunga katika kiwango hiki.

Katika *Bahari ya Elimu ya Ushairi* muundo wa *msitsitizo* umetamalaki katika shairi la ***Pambo la mke (uk.128-130)*** na shairi la ***Nyanyaso la jinsia (uk.131- 132).*** Katika mashairi hayo mawili Andanenga anatumia muundo wa msisitizo wenye mistari mitano *(Takhmisa)*. Katika ubeti wa kwanza wa shairi la ***Pambo la mke*** na ubeti wa kwanza katika shairi la ***Nyanyaso la jinsia*** mtunzi anaonesha;

**Risala piga mdundo, andama njia ufike**
**Kipawa kwa ndugu Shindo, mpe wasia ashike**
**Ni hidaya *aiweke***
***Aiweke* ni upendo, naomba umfunike**
**Pambo halipambi mke, mke hulipamba pambo.**

**Buruji naivuvia, sauti mbali ifike**
**Watakaoisikia, naomba waadilike**
**Mwendo huu *utufike***
***Utufike* kutumia, mwendo mwema tuushike**
**Bila mtoto wa kike, mume atazaliwaje?**

Katika kitabu cha *Bahari ya Elimu ya Ushairi* mwandishi amejitokeza na kutumia muundo wa *ngonjera*. Mtindo wa ngonjera ulibuniwa na Hayati Mathiasi Mnyampala kupitia vitabu vyake viitwavyo *Ngonjera za Ukuta I na II (1969, 1971, 1978).* Ngonjera ni ushairi uliozoeleka kutoa mafunzo kwa jamii. Aghalabu ngonjera huwa na mdadisi na mtoa jawabu. Mtindo wa ngonjera ni ushairi wa kujibizana kati ya watu wawili au zaidi ambao wanajibizana katika hoja fulani na aghalabu mwisho hufikia muafaka katika hoja yao. Andanenga kwa dhamira yake ya kutaka kuendeleza ushairi wa Kiswahili kimuundo hakusita kuutumia. Katika kitabu cha *Bahari ya Elimu Ushairi*, Andanenga anatufunza kuwa ngonjera kwake yeye ni aina ya mchezo unaokusudia kuwachekesha watazamaji na wasikilizaji pia wakati huo huo kuwafundisha. Hebu tuone mfano kutoka ngonjera ya ***Wakati gani hunawa (uk.113-1141)*** ambapo mshairi anaandika hivi:

**Swali:**
**Rafiki mwenye akili, nikuulize suala**
**Njaa imekukabili, nusu ya mwezi hujala**
**Ukute kombe la wali, umewekewa mahala**
**Hunawa mwanzo ukala, hula ndipo ukanawa?**

**Jibu:**
**Njaa ni nusu ya ndwele, na chakula ndiyo dawa**
**Haipoi sharti nile, halafu ndipo tapowa**
**Chakula kiwekwe pale, makusudi nimepewa**
**Nala kwanza n'tanawa, baada ya kwisha kula.**

Ngonjera ya hapo juu imetungwa kwa mtindo wa kujibizana beti kwa beti kwa mwendo wa shairi: 8/8, *tarbiya.* Katika hali tofauti mshairi anonesha kuwa ngonjera huweza kuimbwa na watu wawili kwa kutumia ubeti mmoja tu kila mmoja hadi mwisho wa ngonjera. Lakini kila mmoja akitumia kipande kimoja cha mshororo.Tuone mfano mwingine ufutao katika ngonjera ya ***Bwana na Mke (uk.114-115)*** pale walipojibizana:

**Bw: Uhali gani azizi, Mk: hali yangu njema bwana**
**Bw: Khabari za matembezi, Mk: kwa kweli salama sana**
**Bw: Wa 'hali gani wazazi, Mk: wote wazima kibwana**

**Wote:**
**Twashukuru kukutana, sisi wapenzi wawili**
**Baada ya kutengana, kwa kuishi mbalimbali.**

Katika mfano wa ngonjera tuliouona utagundua kuna ufundi mkubwa wa kifani uliotumika. Umbo la ngonjera hiyo lipo katika mwendo wa 8/8, *tathlitha* na kila kipande katika mshororo ndicho kinachosemwa na mtambaji hadi mwisho wa ubeti. Kisha watambaji huunganishwa na kibwagizo kimoja chenye mistari miwili *(mathna)* katika mwendo wa shairi: 8/8. Ngonjera haikupoteza vina na mizani. Huu ni ubunifu wa kipekee katika ngonjera.

Kadhalika katika kitabu cha *Bahari ya Elimu ya Ushairi*, mtunzi ametuonesha namna ya kutunga ngonjera ya mshororo kwa mshororo. Huu ni mtindo wa utunzi wa ngonjera ambao kila mtambaji hutamba na mstari wake katika kukamilisha hoja yake. Mfano kutoka ngonjera nyingine ya ***Bakari na Ali (uk.116-117)*** inasema hivi:

**B: Hodi hodi bwana Ali, hodi ndani samahani!**
**A: Karibia tafadhali, karibu ingia ndani**
**B: Nakushukuru kikweli, kwa karibu ya hisani**
**A: Umetoka huko mbali, azma yako ni nini?**

Katika mfano huo itabainika na kugundua kuwa kila muhusika kati ya Bakari (B) na Ali (A) anatamba na mstari mmoja katika majibizano yao hadi kukamilisha ubeti. Pamoja na kutokuwa yeye Andanenga si mwasisi wa ngonjera, ameweza kuunogesha zaidi mtindo huu wa mashairi kwa kuongeza maumbo mengine ya kisanaa na kimaudhui huku akienda mbali zaidi ya mwasisi Mathiasi Mnyampala ambaye yeye beti zake nyingi zimo katika mwendo wa shairi: 8/8 wa *tarbiya.*

Katika *Bahari ya Elimu ya Ushairi*, Andanenga amefinyanga shairi kwa mtindo wa *Ukawafi.* Andanenga (2002:42) anaeleza kuwa *Ukawafi* hutungwa kwa mpango wa mizani kumi na tano katika kila mstari (Mshororo) na kuwa na kituo baada ya mizani sita na ya tano, au baada ya sita tu (6/4/5 au 6/9). Ni mtindo wa zamani sana unaoaminika kuwa ulitumiwa hasa kwa ajili ya mashairi ya kidini. Muundo wa ukawafi hutumiwa pia kwa ajili ya mashairi yasiyo ya kidini. Hebu tuone mfano ufuatao wa ukawafi ukiwa katika muundo wa shairi lenye mistari miwili *(Mathna)* katika mwendo wa 6/4/5 kila ubeti ukiwa na mistari miwili na kina ni ***-ma*** lililotungwa na Shehe Mohammad al- Azabii (uk.42-43) kama alivyonukuliwa na mwandishi wa kitabu linasema:

**Nahimidi mungu kwa himidi ilotukuka**
**Thumma salawatu ‘alaihi wa tasilima.**

**Waloumba mbingu aunaka yaa Mu’imu**
**Kwa utungo huno niweleze uwe timama**.

Kadhalika mtindo wa *ukawafi* huweza pia kutungwa katika muundo wa *tarbiya* likiwa katika mwendo wa shairi la 6/4/5 na kukamilisha idadi ya mizani kumi na tano katika mstari. ***Ukawafi wa Miiraji (uk.43)*** uliotungwa na Andanenga, katika ubeti wa kwanza unaimbika hivi:

**Nanza kunudhumu, kwa isimu, yake Karima**
**Mola muadhamu, mtukufu, mwenyi rehema**
**Hazina ukomu, swifa zake, mwenyi adhama**
**Sala na salamu, na mbawazi, zendee Tuma.**

Katika ubeti huo utagundua kuwa mistari mitatu ya kwanza ina kina na mstari wa nne wa beti zote ni bahari na kina ni ***-ma***. Vipande havina kina maalum.

Sambamba na hilo, *ukawafi* huweza kutungwa katika muundo wa mashairi yenye mistari mitano *(Takhmisa).* Katika *Bahari ya Elimu ya Ushairi* mtunzi ametuonesha muundo huo kupitia shairi la ***Tutende Mema (uk.53)*** likiwa katika mwendo na umbo la mizani 6/9 katika kila mstari. Umahiri wa mshairi katika ubeti w tano wa shairi unasema hivi:

**Yangu kaditama, yasisitiza wote sisi**
**Twahimizwa wote, kwa kuyaachia maasi**
**Ataporidhika, Ya Allahu Mola Mkwasi**
**Janna ndiyo yetu, ni malipo yenye nemsi**
**Mola utujaza, tukakae bila kutoka.**

Katika ubeti huo tunaona mwandishi akionesha namna ya kutunga mtindo wa ukawafi katika umbo la mistari mitano likiwa katika mwendo wa 6 na 9. Katika ubeti huo kuna kipande cha kwanza cha mstari kina mizani sita na kipande cha pili

kina mizani tisa. Lakini utaonekana kuwa kipande cha kwanza cha kila mstari hakina kina lakini kipande cha pili katika mstari kinaishia na kina ***-si*** katika ubeti mzima.

Kadhalika katika kuendelza ushari wa Kiswahili kimuundo Andanenga katika kitabu chake cha *Bahari ya Elimu ya Ushairi* amekuja na mtindo wa *Wajiwaji*. Hii ni aina ya shairi ambalo hutumiwa na mshairi ili kujieleza au kujisifu mwenyewe (Andanenga, 2002:44). Aina hii ya ushairi pia hutumiwa kwa ajili ya kutoa waadhi na maonyo. Sura ya asili ya *Wajiwaji* huenda ni *nyingi.* Wajiwaji inaweza kuwa katika umbo la *Mathna* au *Takhmisa* na inaweza pia kuwa katika mwendo wa *Ukawafi* au *Dural- mandhuma*. Shairi la ***Wajiwaji (uk.54-55)*** twaliona likiwa pia na mwendo wa *ukawafi* na *Dural- mandhuma* katika ubeti wa kwanza na wa pili:

**Wajiwaji wangu, nautunga, kwa makusudi**
**Kwa mahaba yangu, Andanenga, Amiri Sudi**
**Someni wenzangu, nalopanga, zake idadi**
***(Alifu)* – *A*lo na matungu, iwe kinga, kwenye fuadi,**
**Mbele yake Mungu, baya janga, likubaidi.**

**Uwe mwongozo, kwetu wote, tutaosoma**
**Yake maelezo, yatupate, Baba na Mama**
**Na matekelezo, yafuate, bila kugoma**
**(*Ba*) – *Ba*raka kwa mzo, tuzipate, kesho kiama**
**Tupate uwezo, siku zote, tupe wadudi.**

Shairi hili linadhihirisha uwezo alionao mwandishi katika kutumia miundo na mitindo anuai katika fani na sanaa ya ushairi wa Kiswahili. Hivyo kuzidi kuupa uhai na maendeleo uga huu hasa katika kipengele cha muundo.

Vilevile Andanenga katika kitabu cha *Bahari ya Elimu ya Ushairi* amejaribu kutumia mtindo wa *Duril- mandhuma*. Mbinu za duril-mandhuma (au akirostika) hutungwa mara nyingi katika mwendo wa *kisarambe* (Andanenga, 2002:59). Mwandishi anaendelea kudadadvua kuwa; ushairi wa mizani kumi na moja umepanda katika fani

yake hadi kufikia utungo wa kiwango cha haiba zaidi katika herufi za maandishi ya Kiarabu. Zipo irabu kuu tatu katika lugha ya Kiarabu nazo ni ***Fataha, Kisra*** na ***Dhuma*** yaani ***a- i -u***. Kutokana na herufi hizo, Andanenga anadai kuwa, Sheikh Omar Bin Amin ambaye inasemekana alikuwa kipofu katika shairi lake la *duril-mandhuma* ametunga kufuatana na jinsi ya herufi zenyewe zilivyo na irabu zake kuanzia ***alif, bee, tee*** hadi ***yee*** kama ifuatvyo:

**Alifu. alifu fataha "*a*"**
**Andika mwandishi hati utuze**
**Alfu kisira *"i"***
**Isimu ya mola utangulize**
**Alifu dhuma *"u"- a, -i, -u***
**Utiye nukuta na irabuze**
**Wasikulaini wenye kusoma.**

**Be. bee fataha *"ba"***
**Baada ya ina kulibutadi**
**Bee kisra *"bi"***
**Bijahi Rasuli tumuhimidi**
**Bee dhuma *"bu" -ba -bi-bu***
**Bushira ya pepo naswi tufidi**
**Mola atujazi majaza mema.**

Andanenga (2002:60) anatueleza kuwa huo ni mfano wa namna ya usomaji. Lifuatalo ni shairi kamili kuanzia ***alifu*** mpaka ***yee***. Tuone mfano wa ubeti wa kwanza na wa pili (uk. 60-65) wa shairi hili likiwa katika muundo na mwendo wa mizani kumi na moja kama hivi:

**Alifu-**
**Andika mwandishi hati utuze**
**Isimu ya mola utangulize**
**Utiye nukuta na irabuze**
**Wasikulahini wenye kusoma.**

**Bee-**
**Baada ya ina kulibutadi**
**Bi jahi Rasuli tumuhimidi**
**Bushira ya pepo nasi tufidi**
**Mola atujazi majaza mema.**

Muundo kama huu pia umetumika katika diwani ya *Kale ya Washairi wa Pemba (Abdulla, M., 2011:70)* akitumia shairi la ***Rabi Ondoa Nakama***.

Kadhalika Andanenga ameweza pia kutunga *duril- mandhuma* kwa kutumia herufi za Kiarabu katika muundo wa *kisarambe* yaani mizani kumi na moja katika mwendo wa shairi: 6/5. Hebu tuone mfano wa shairi lifutalo *(uk.68-70)* ambalo limetungwa na Andanega:

**Da- Daima haina, Dunia hii**
**Di- Dini ya Rabbanna, bora kutii**
**Du- Dunia fitina, usiitii**
**Siishangilii, haina uzuri.**

**Ra- Raha yenye kweli, haipo hapa**
**Ri- Ridhiya kauli, ninayokupa**
**Ru- Rudia halali, haramu kwepa**
**Pia kumwogopa, Mungu Jabbari.**

**Sa- Sasa takomea, nikipotosha**
**Si- Si kunizomea, kisahihisha**
**Su- Sudi tachekea, kweli maisha**
**Hunifurahisha, mimi Amiri.**

Baada ya kuona mfano wa shairi hilo hapo juu lenye muundo wa mizani kumi na moja katika mtindo wa *kisarambe* kwa kutumia hati za Kiarabu kama vile ***-a -i -u***

katika ubeti wa kwanza na ***ba -bi -bu*** katika ubeti wa pili. Mtunzi ameenda mbali zaidi katika kudhihirisha uwezo wake wa kucheza na miundo mbalimbali ya ushairi wa Kiswahili pale anapotunga Durili-mandhuma katika akirostika za kirumi. Katika shairi la ***Dura Li- mandhuma (uk.66-67)*** katika mwendo wa shairi: 6/5 ya *kisarambe* katika umbo la *takhmisa* mtunzi anathibitisha hilo katika beti zifuatazo:

**A -Allah lako jina, natanguliza**
**E-Ewe subuhana, tupe mwangaza**
**I-Ili yake janna, kutuingiza**
**O - Onyesha bayana, ya kupendeza**
**U - Utupe ruwaza njema ahadi**

**Ba- Baada ya mungu, kukuhitaji**
**Be- Beti hizi zangu, zipe mtaji**
**Bi- Bidii si zangu, zako mpaji**
**Bo- Boresha mafungu, kwa wasemaji**
**Bu- Busara za mbiji, tupe abadi.**

Katika beti hizo mtunzi ameonesha ubingwa wa kuweza kutufunza jinsi ya kutunga mashairi katika mtindo wa *duril-mandhuma* akituelekeza namna ya kutumia herufi za Kiarabu huku akinukuu baadhi ya mashairi ya washairi wengine. Lakini Andanenga ameenda mbali zaidi akitunga kwa kutumia herufi na irabu za Kirumi.

Katika ubeti wa kwanza mwandishi anatumia irabu za *-a -e -i -o -u* katika uanzaji wa mshororo hasa katika kipande cha kwanza na katika ubeti wa pili anatumia silabi za *-ba -be -bi -bo -bu* katika uanzaji wa mstari hasa katika kipande cha kwanza cha mshroro. Mtririko huo huendelea kwa herufi nyingine kwa mfuatano wake wa kimantiki hadi mwisho wa shairi.

## 4.4 Hitimisho

Imebainika kuwa Andanenga ni shaha wa ushairi wa Kiswahili wa kiwango cha juu sana. Mwandishi huyu ameweza kuambaa na kudhihirisha miundo anuai ya ushairi wa Kiswahili. Mtunzi hakuwa mbali na dhana halisi ya ushairi wa Kiswahili, kwani kupitia miundo anuai ya ushairi ameweza kuibua, kushadidia na kubainisha mitindo mbalimbali ya ushairi wa Kiswahili ambayo haiachani kabisa na kanuni na arudhi za uandishi wa mashairi ya kimapokeo ambayo mtunzi ni mfuasi wake. Kwa maana hiyo basi, miundo na mitindo changamani iliyojadiliwa katika utafiti huu imeshikana na kuumana sana na nadharia ya umuundo ambayo ndiyo iliyoongoza katika kubaini mchango wa kimuundo wa Andanenga katika kuuendeleza ushairi wa Kiswahili. Hakika mchango wake mpana ni mkubwa katika ushairi wa Kiswahili kimuundo.

# SURA TA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii imejikita katika kutoa hitimisho la utafiti huu kuhusu Mchango wa Amiri Sudi Andanenga katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili. Mambo yaliyomo katika eneo hili ni pamoja na utangulizi wa sura hii. Sehemu ya pili imetoa maelezo mafupi kuhusu utafiti ili kusisitiza malengo na umuhimu wa utafiti huu. Sehemu ya tatu inahusu majumuisho ya matokeo yaliyopatikana kulingana na malengo ya utafiti. Sehemu ya nne imeelezea mchango wa utafiti huu na sehemu ya tano imebainisha maeneo yanaoyohitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

## 5.2 Muhutasari wa Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kubainisha mchango wa Andanenga katika ushairi wa Kiswahili. Malengo ni kubainisha mchango wake wa kidhamira na kimuundo katika ushairi wa Kiswahili. Katika sura ya kwanza, mtafiti ameanza kwa utangulizi akieleza kwa kifupi Usuli wa tatizo la utafiti. Mtafiti ameeleza kwa kifupi juu ya chimbuko na historia ya ushairi wa Kiswahili. Hatimaye sura imejikita katika kuangazia historia ya maisha ya Amiri Sudi Andanenga. Vipengele vingine muhimu vilivyobainishwa ni tamko la utafiti, malengo ya utafiti, tija na umuhimu wa utafiti, maswali ya utafiti, mawanda ya utafiti na mpango wa utafiti.

Sura ya pili, imejikita katika kuangalia mapitio ya maandiko. Mapitio hayo yanazungumzia juu ya dhana ya ushairi, dhamira na muundo katika ushairi ambayo yamezingatiwa. Hata hivyo, maandiko mengine yenye mnasaba na yanayoelekeana

na kazi ya utafiti yamepitiwa. Sura ya tatu imejielekeza katika kubainisha mbinu na vifaa vilivyotumika katika utafiti huu. Vipengele vilivyojumuishwa katika sura hii ni pamoja na; uchambuzi wa data, vifaa, mbinu na vyanzo vya kukusanyia data, mbinu za kupata sampuli, sampuli ya watafitiwa, mahali pa utafiti na nadharia za utafiti.

Sura ya nne, imejielekeza katika uchambuzi na uchanganuzi wa data za matokeo ya utafiti. Vipengele vilivyojumuishwa katika sura hii ni maelezo kuhusu vitabu teule, mchango wa kidhamira wa Andanenga katika ushairi wa Kiswahili na hatimaye mchango wa kimuundo wa Andanenga katika ushairi wa Kiswahili.

Sura ya tano inamalizia katika kutoa hitimisho ya mambo yote kwa muhutasari katika utafiti huu. Mapendekezo ya mambo yanayotakiwa kufanyiwa utafiti, juu ya Andanenga yamebainishwa. Mshairi huyu imebainika kuwa hajafanyiwa tafiti za kutosha kama washairi wengine wa zama zake ingawa ana mchango mkubwa katika ushairi wa Kiswahili. Mbali na hivyo, matokeo, mchango na maoni ya utafiti yamebainishwa katika sura hii.

### 5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huibuliwa na kile kilichokusudiwa kutokana na malengo ya utafiti husika. Matokeo hayo ni muhimu kuendana na maswali yaliyokuwa dira ya utafiti kujibiwa. Utafiti huu ulilienga kutafiti mchango wa Andanenga katika ushairi wa Kiswahili. Aidha utafiti huu ulikusudia kujibu maswali mawili mahususi ambayo ni: nini mchango wa kidhamira wa Andanenga katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili na nini mchango wa kimuundo wa Andanenga katika kuendeleza ushairi wa kswahili. Utafiti umeweza kujibu maswali hayo kinagaubaga kwa kuzingatia pia malengo ya utafiti. Utafiti umebaini dhamira anuai zilizojitokeza katika *Diwani ya*

*Ustadh (1993/2001)* na *Bahari ya Elimu ya Ushairi (2002).* Hii inatokana na ukwele kuwa katika uchambuzi wa dhamira imejionesha namna ambavyo Andanenga amekusudia kueleimisha jamii yake kupitia ushairi wa Kiswahili. Katika ubainishaji huo, ni wazi kuwa mshairi huyu alinuia kuiasa na kuionya jamii yake. Hakika mafundisho anayoyatoa Andanenga ni ya msingi kwa jamii.

Si hivyo tu, utafiti huu umeweza kubaini mzo wa miundo na mitindo mbalimbali ya ushairi wa Kiswahili katika mashairi ya Andanenga. Katika utafiti huu, imedhihirika dhahiri kuwa miundo na mitindo ya ushairi wa Kiswahili ipo mingi, hutegemea sana ubingwa na umahiri wa mtunzi mwenyewe. Andanenga amefaulu katika hilo. Ukiangalia ndani ya *Bahari ya Elimu ya Ushairi (2002)* mtunzi huyu amemudu kuzama katika kina kirefu cha bahari hiyo kwa na kututanabahisha miundo na mitindo mbalimbali ya ushairi wa Kiswahili.

Mwisho, utafiti huu umeoneshai kuwa mwandishi Andanenga ametoa mchango mkubwa katika ushairi wa Kiswahili. Pamoja na kuwa na mchango wake mkubwa katika ushairi wa Kiswahili, bado mshairi huyu hajapata kuandikwa habari zake kama waandishi wengine wa kabla na wakati wake akiwamo Shaaban Robert, Saadan Abdu Kandoro, Kaluta Amri Abeid na Mathias Mnyampala. Utafiti huu ni mchango wa awali katika azma hiyo.

## 5.4 Mchango wa Utafiti

Shabaha ya tafiti zote ni kutatua na kuleta suluhisho la tatizo mahususi. Mchango wa utafiti huu, umewezesha kufikiwa kwa lengo la utafiti huu ambao lilikuwa ni kushughulikia mchango wa kidhamira na kimuundo katika ushairi wa Andanenga. Mchango wa utafiti huu ni kuwa umeibua na kuonesha namna ambavyo katika ushairi wa mtafitiwa kuna mchango mkubwa wa kidhamira na kimuundo.

Dhamira kadha wa kadha za uzalendo, pendo la pesa, wema, mapenzi ya dhati, dini, umbea, haki ya kupiga kura, utamduni, kuhusu ushairi na Kiswahili, Heshima kwa wazazi, uchumi na utamaduni yamejadiliwa. Katika ubainishaji huo ni wazi kuwa dhamira hizo zimesadifu na kuakisi mazingira halisi ya jamii yetu. Kwa mnasaba huo mshairi huyu alinuia kuiasa na kuionya jamii yake ili iweze kuishi maisha ya usawa na usitawi. Bila ya shaka matokeo ya kusomwa kwa mashairi hayo yenye dhamira anuwai mwamko umepatikana kwa jamii.

Mchango mwingine wa utafiti huu umeibua na kudhihirisha wazi miundo na mitindo mbalimbali katika ushairi wa Kiswahili. Hii inatokana na ukweli kwamba katika uchambuzi wa mashairi ya Aandanenga, miundo kama vile; *Sudusia*, *takhmisa*, *tarbiya*, *tathlitha* na *mathna* imeweza kubainishwa. Kadhalika mitindo ya ushairi kama *wajiwaji*, *ukawafi*, *gungu*, *duril-mandhuma*, *mtiririko*, *msisitizo* na *ngonjera* nayo iliweza kuibuliwa. Mitindo hii yaweza kuwa chachu ya kuibuliwa mitindo mingine mipya na kutumika. Matokeo yake hazina ya ushairi itaimarika.

## 5.5 Maoni ya Mtafiti

Utafiti huu ulijikita katika kubaini mchango wa kidhamira na kimuundo katika ushairi wa Andanenga. Pamoja na hayo, imedhihirika wazi kuwa mchango wake katika sanaa ya ushairi ni mkubwa. Historia yake inabainisha wazi kuwa mwandishi huyu anapenda kuendeleza na kutumia utamduni wake, hususani lugha ya Kiswahili na ushairi wake. Katika utafiti huu imebainika kuwa Andanenga ana mchango mkubwa katika ushairi wa Kiswahili kidhamira na kimuundo. Ni kwa sababu hiyo basi, njia pekee ya kuendeleza lugha na ushairi wa Kiswahili ni kuhifadhi mchango wake kwa njia ya maandiko.

Kadhalika, mtafiti anashauri kuwa Vyuo Vikuu vyote vinavyotoa shahada za ngazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili vitengeneze kozi ya pamoja itakayokuwa inafundisha ushairi wa Kiswahili na maisha yao. Kwani kwa sasa ni washairi wachache wanaosomwa katika kozi maalumu.

Hivi sasa mshairi huyu hana mtu wa kutunza nyaraka zake za kifasihi kutokana na watoto wake kutokuwa na mapenzi na sanaa hii ya ushairi. Kwa maoni ya mtafiti, anashauri wengine kama vile watafiti, wasomi na wapenzi wa lugha na fasihi ya Kiswahil wafanye jitihada za kukusanya kazi za msanii kwa ajili ya tafiti na kuweka katika makavazi.

## 5.6 Mapendekezo kuhusu Tafiti Zijazo

Utafiti huu umelenga kubainisha mchango wa Andanenga katika ushairi wa Kiswahili. Umejiegemeza zaidi katika kuangalia mchango wake wa kidhamira na kimuundo wa mshairi huyu. Mpaka sasa, inaaminika kuwa kazi hii ni ya kwanza

katika kuchunguza mchango wa kidhamira na kimuundo katika ushairi wa Andanenga.

Utafiti huu haukuweza kujibu kila kitu katika kuangalia mchango wa Andanenga katika ushairi wa Kiswahili. Watafiti wengine wajao waweza kupata mwelekeo wa kutafiti zaidi maeneo mengine ya ushairi katika ushairi wa msanii huyu kwa kuangalia vipengele vya kifani kama vile taswira na ishara, jazanda na tamathali za semi. Ama waweza kuangalia falsafa na itikadi katika maudhui ya mashairi ya Andanenga. Shughuli hiyo itatoa mwanya wa kuangalia namna Andanenga alivyojaaliwa ujuzi na upekee katika uwanja wa sanaa ya ushairi. Hata hivyo, utafiti huu waweza kuwa mwendelezo wa kuangalia mchango wa washairi wengine na kazi zao.

**5.7 Hitimisho**

Kwa kuhitimisha sura hii, mtafiti anapendekeza watafiti wajao waendelee kutalii vipengele mbalimbali katika maisha na kazi za kisanaa za Amiri Sudi Andanenga na washairi wengineo ili kuweza kubaini mengi ambayo hayajulikani kwa jamii hii leo kuhusu washairi na ushairi wa Kiswahili. Kufanya hivyo, kutasaidia kuibua na kuonesha wazi mchango wao katika kuendeleza sanaa ya ushairi wa Kiswahili.

## MAREJELEO


Abdallah, A (1973), "Ushairi wa Kiswahili: Nauhuisha usiuliwe", *Zinduko I,* Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Abedi, A (1954), *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri,* East African Literature Bureau, Nairobi.

Andanenga, A.S (1993), *Diwani ya Ustadhi,* Benedict Publication, Ndanda-Peramiho.

____________ (2002), *Bahari ya Elimu ya Ushairi,* Benedict Publication, Ndanda-Peramiho.

Akilimali, S.W (1966), *Diwani ya Akilimali*, East African Literature Bureau, Nairobi.

Barthes, R (1988), *Structuralism and Semiotics,* Macmillan Pr, London.

Bhalo, J.A (1977), "Muyaka wa Muhaji na Ushairi wa Kiswahili", *Mulika Na 10:1-13*, TUKI, Dar es Salaam.

Bukagile, R, (2008), *Kiswahili kidato cha 3 na 4,* Nyambari Nyangwine Publishers, Dar es Salaam.

Chiraghdin, S (1970), *Utangulizi*: *Malenga wa Mvita*, Oxford University press, Nairobi.

__________ (1987), *Malenga wa Karne Moja*, Longman, Nairobi.

Chamba, L.A (2011), *Dhamira Kwenye Nyimbo za Wasanii Wasioona na Mtazamo wao kwa Jamii:* Tasnifu ya Kukamilisha Shahada ya uzamili katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (Haijachapishwa).

De Saussure, F (1993), *A Course in General Linguistics,* Pergamon Press, Oxford.

Durey, J.F (1993), *Realism and Narrative Modality*, Gunter Narr Verlag, Tuebingen.

Fried, M (1987), *Realism, Writing, Disfigurations:* On Thomas Eakins and Stephen Crane, The University of Chicago Press, Chicago.

Gibbe, A.G (1978), *Shaaban Robert: Mshairi,* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.

___________ (1995), "*Inkishafi*" *Uhakiki wa Kidiakronia*, Tasnifu ya Kukamilisha Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Moi Eldoret, Kenya (Haijachapishwa).

Kant, I (1928), *Critique of Judgment*, trans. James Creed Meredith, Clarendon Press, Oxford.

Kessel, V.L (2001), *Dibaji: Bahari ya Elimu ya Ushairi*, Benedict Publication, Ndanda- Peramiho.

Kezilahabi, E (1976), *Ushairi wa Shaabani Robert,* East .African Literature Bureau, Nairobi.

Kothari, C.R (2008), *Research Methodology: Methods and Technique,* New Age, New Delhi.

Kumar, R (2005), *Research Methodology: A step by step Guide for Biginners,* SAG Publication, Malaysia.

Khatib, M.S (2003), *Wasakatonge,* Oxford University Press, Dar es Salaam.

__________ (2011), *Chanjo, Matakwa ya Mwanamume Katika Mwili wa Mwanamke: Ulinganisho wa Mashairi ya Muyaka bin Haji na Shaaban Robert.*Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Masebo, J. A (2002), *Kiswahili kidato cha 3 na 4*, Afro Industries Ltd, Dar- es-salaam.

___________ (2008), *Jitayarishe Kwa Kiswahili,* Nyambari Nyangwine Publishers, Dar-es-Salaam.

Mayoka, J (1986), *Mgogoro wa ushairi na Diwani ya Mayoka,* Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

_________(1993), *Utangulizi: Diwani ya Ustadh* , Benedict Publicztion, Ndanda-Peramiho.

Mazrui na Shariff, I.N (1975), "A Note on Kiswahili Poetry", *Kiswahili*, TUKI, Dar-es-Salaam.

Morris, P (2003), *Realism, New Critical Idion, Rontledge*, 11 New Fetterlane, London.

Mulokozi, M.M (1989), “Uchambuzi wa Mashairi”, *Mulika Na 21:50-51*, TUKI, Dar-es- salaam.

Mulokozi, M na Kahigi, K (1974), *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Mushengyezi, A (2003), 20th *Centuary Literary theory*, Mukono Bookshop Priting and Publishing Company Ltd., Kampala.

Mnyampala, M.E (1965), *Diwani ya Mnyampala*, East Africa Publication, Arusha-Dar es Salaam.

______________ (1969), *Ngonjera za Ukuta I na II*, Oxford University Press, Dar es salaam.

______________ (1971), *Waadhi wa Ushairi*, Oxford University Press, Dar es salaam.

Mhilu, G (2008), *TAHAKIKI, Vitabu Teule vy Fasihi Kidato cha 3 na 4, Nadharia Uhakiki na Maswali:* Nyambari Nyangwine Publishers, Dar- es-Salaam.

Mwinyi, A .H (2001), *Utangulizi: Bahari ya Elimu ya Ushairi*, Benedict Publicatio, Ndanda-Peramiho.

Ndulute, C (1994), *The Poetry of Shaaban Robert*, Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam.

Nassir, A (1970), *Malenga wa Mvita*, Oxford University Press, Nairobi.

Njogu, K na Chimera, R (1999), *Ufundishaji wa Fasihi*, Jommo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Olson, S.H (1975), “Philiosophical Implications of Some Swahili Idioms”, in *Kiswahili Vol 45/2:32-37,* TUKI, Dar-es- Salaam.

Robert, S (1958), “Hotuba Juu ya Ushairi”, *Journal of East African Swahili Committee,* Na. 28/1:37-41, Dar es Salaam.

____________ (1966), *Pambo la Lugha*, Oxford Universty Press, Dar es Salaam.

_____________ (1970), *Sanaa ya Ushairi*, Thomas Nelson, Nairobi.

____________ (1973), *Kielelezo cha Fasili*, Thomas Nelson, Nairobi.

Sanka, S.M (1994), *Semantic Deviation in Iraq Poetry*, M.A Dessertation (Unpublished) UDSM.

Senkoro, F.E.M.K (1982), *Fasihi,* Press and Publicity Centre, Dar es Salaam.

Shaaban, N (2009), *Kiswahili Shule za Sekondari Kidato cha Nne,* Oxford University Press Tanzania Ltd, Dar es Salaam.

Snow, C. P (1968), *The Realists:* Potraits of Eight Novelist, Macmillan, London.

Takiluki, (1997), *Malenga Wapya*, Oxford University Press, Dar es Salaam.

Tallis, R (1998), *In Defence of Realism*, Bison, U.S.A.

Todorov, T (1977), *The Poets of Prose,* Oxford, London.

Warren, A na Wellek, R (1985), *Theory of Literature*, Penguin Groue, London.

Wellek, R (1960), *The concept of Realism in Literature Scholarship*, Neophilologues Ltd, London.

# VIAMBATISHO

## I. Hojaji kwa ndugu, jamaa, na marafiki wa Amiri Sudi Andanenga

1. Je, unaweza kueleza historia ya maisha yako kwa ufupi? Kwa mfano, jina lako, umri wako, mahali unapoishi n.k.
2. Unamfahamu vipi Amiri Sudi Andanenga?
3. Je, unazifahamu kazi alizoandika Amiri Sudi Andanenga? Zitaje?
4. Je, kuna kazi nyingine alizoandika Amiri Sudi Andanenga ambazo hazijachapwa? Ni zipi hizo?
5. Una maoni gani kuhusu hadhi ya mwandishi huyu hapa nchini?
6. Unafahamu chochote kuhusu mashairi ya mtiririko na msisitizo? Je mtunzi alishawahi kutumia muundo huu wa utungaji?(washairi)
7. Je, unafikiri ni mtunzi gani aliyemuathiri Amiri Sudi Andanenga katika utunzi wa mashairi ya mtiririko na msisitizo?(washairi)
8. Unaweza kutueleza mashairi ya Andanenga yanajadili kuhusu nini zaidi?na kwa nini?(washairi)
9. Je, alishirikiana vipi na washairi wengine?(washairi)
10. Unamzungumziaje Andanenga na UKUTA?(washairi)

**II. Hojaji kwa washairi**

1. Unadhani Amiri sudi Andanenga ana mchango wowote wa kimaudhui katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili?
2. Una mawazo gani kuhusu suala la uzalendo unapomuangalia Amiri Sudi Andanenga?
3. Kuna madai kuwa baadhi ya waandishi wanajibainisha kama wanasiasa; wewe unampa nafasi gani Amiri Sudi Andanenga huku ukiyaakisi maandishi yake kwa jumla? Kwa nini?
4. Unawezaje kuihusisha dhana ya uwanamapinduzi na kazi za Amiri Sudi Andanenga ulizosoma au kuhakiki?
5. Unamzungumzia vipi Amiri Sudi Andanenga kuhusu lugha ya Kiswahili?
6. Je, kuna harakati zozote unazozifahamu kuhusu mwandishi huyu katika kuusemea au kuuhami ushairi wa Kiswahili?
7. Unadhani Amiri Sudi Andanenga ana mchango wowote wa kifani hasa katika kipengele cha muundo katika kuendeleza ushairi wa kiswahili?
8. Mwandishi kuwa athura wa kazi za mwandishi mwingine si jambo geni. Unafikiri ni waandishi wepi wa zama hizi walioathiriwa na uandishi wa mashairi wa mtunzi huyu?
9. Unasemaje kuhusu muundo wa mashairi ya Amiri Sudi Andanenga?

**III. Hojaji kwa mtunzi mwenyewe**

1. Je, mzee Andanenga ulizaliwa lini na wapi?
2. Ni wa ngapi kwa kuzaliwa na ulizaliwa na ndugu wepi wengine?
3. Wazazi wako waliitwaje? (Majina ya Baba na Mama), ni wenyeji wa wapi?
4. Ulisoma shule gani ya msingi, ya kati na sekondari?
5. Ulimaliza shule lini?
6. Unaweza kutueleza kazi ulizofanya, wapi na lini?
7. Unaweza kutueleza ulioa lini na ulimuoa nani?
8. Je, mlijaaliwa kupata watoto? Wangapi? (wataje kwa majina)
9. Je, kuna wajukuu na vitukuu?
10. Je, ulianza lini kutunga mashairi? Unalikumbuka shairi lako la mwanzo?
11. Ulishawahi kuishi kama mwanasiasa nje na ndani ya ushairi wako? Kwa vipi?
12. Ulishirikiana vipi na washairi wengine?
13. Vipi kuhsu UKUTA? Una harakati zozote?
14. Je, kuna mtoto au ndugu wa karibu anayeonekana kurithi kipaji chako?
15. Kishairi, unaweza kutueleza ni watunzi gani wa kabla na wakati wako waliokuathiri katika utunzi wako?
16. Vipi kuhusu lugha ya Kiswahili? Ushafanya harakati zozote kuitetea?
17. Je, kuna zawadi na tunzo zozote ambazo ulishapata kupitia ushairi wako?
18. Vipi kuhusu malumbano ya ushairi? Yana tija yoyote katika ushairi wa Kiswahili?
19. Je, ulishawahi kutoa mada kuhusu taaluma ya ushairi? Wapi?
20. Mambo gani huvutiwi nayo?
21. Wewe ni mlevu wa kuona, uliupataje?
22. Katika hali hiyo changamoto gani hukukabili za kifamilia na kisanii.
23. Washairi gani wamekuvutia na kukuathiri na kwa nini?
24. Nini maoni yako juu ya ushairi wa kimapokeo wa vina na mizani na mashairi ya kisasa?
25. Uandishi wa mashairi unakupatia mapato na tija?

**IV. Baadhi ya vyeti alivyotunukiwa**

Certificate of merits, mwaka 2002, kwa mchango wake wa lugha na fasihi.



**Cheti cha Heshima, katika kukieneza na kukienzi Kiswahiuli katika fani ya ushairi.**



**V.Orodha ya watu waliohojiwa katika utafiti huu**

i. Mzee Ramadhani Kaniki – Mshairi (Dodoma).

ii. Rashidi Mkonikoni – Mshairi (Dodoma).

iii. Juma Nyembe – Mshairi (Dodoma).

iv. Rashid bin Rashid Mfaume – Mshairi (Morogoro).

v. Tatu binti Saadala – Mke wa Andanenga.

vi. Nadhija binti Amiri – Mtoto wa Andanenga.

vii. Saidi bin Amiri – Mtoto wa Andanenga.

viii. Selemani mvomvo – Mwanafunzi shahada ya Uzamili UDOM (2011/2012).

ix. Gervas Kasiga – Muhadhiri Chuo Kikuu cha Dodoma.